


esperanto

Nino Vessella



esperanto
Jifunze lugha ya kiesperanto

ilei

Nino Vessella

1



esperanto

jifunze lugha ya kiesperanto

Eldonisto: ILEI

Eldonjaro: 2021

ISBN: 978-2-940665-00-6

Kvara eldono nove prilaborita

Eldonkvanto: 500

Enpaĝigo: José Roberto Tenorio

Kovrilo: Leandro Abrahão

Provlegado: Prof. Elisée Byelongo Isheloke

Yaliyomo

Ukurasa

Utangulizi 5

Somo la kwanza 7

1. Matamshi, 7. — 2. Mkazo, 8. — 3. Zoezi, 9.

Somo la pili 11

4. Kibainishi, 11. — 5. Uundaji wa maneno, 12. — 6. Kiambishi -O, 13. — 7. Zoezi, 14. — 8. Kiambishi -A, 14. — 9. Zoezi, 16. — 10. Maneno machache, 16. — 11. Zoezi, 16.

Somo la tatu 19

12. Kiambishi awali *MAL*-, 19. — 13. Zoezi, 20. — 14. Kiambishi -J, 20. — 15. Zoezi, 21. — 16. Mifuatano ya maneno -AJ -OJ, 21. — 17. Mfululizo wa vivumishi, 21. — 18. Zoezi, 21. — 19. Kumbuka!, 22. — 20. Neno **ESTAS**, 22. — 21. Jifunze maneno yafuatayo, 22. — 22. Zoezi, 23. — 23. Zoezi, 23.

Somo la nne 25

24. Kitenzi, 25. — 25. Kiambishi tamati -AS, 25. — 26. Mtendaji, 26. — 27. Zoezi, 26. — 28. Zoezi, 27. — 29. Neno *NE*, 27. — 30. Zoezi, 28. — 31. Vihusishi, 28. — 32. *APUD*= karibu na, 28. — 33. *SUB*= chini ya, -ni, 28. — 34. *AL*, 29. — 35. Zoezi, 29.

Somo la tano 31

36. Maswali, 31. — 37. Zoezi, 33. — 38. Misemo akali, 33. — 39. Misemo mingine, 34. — 40. Maswali, 34. — 41. Zoezi,

34. — 42. Kiambishi tamati *-IS*, 35. — 43. Zoezi, 35. — 44. Kikati *-IN-*, 35. — 45. Zoezi, 36.

Somo la sita.37

46. Rangi, 37. — 47. Nambari, 37. — 48. Upangaji wa kivumishi, 38. — 49. Zoezi, 39. — 50. Zoezi, 39. — 51. Viulizi, 40. — 52. Mtendaji na mtendewa, 40. — 53. Zoezi, 42. — 54. Vitenzi akali, 42. — 55. Zoezi, 42.

Somo la saba.43

56. Alama ya mtendewa *-N*, 43. — 57. Upatanishaji wa kisarufi, 43. — 58. Zoezi, 44. — 59. *KI*Ana *KIU*, 44. — 60. Kiambishi tamati *-OS*, 44. — 61. Vielezi vya wakati, 45. — 62. *KIAM*?= lini? wakati gani?, 45. — 63. Zoezi, 45. — 64. Umilikishi, 46. — 65. Vimilikishi, 46. — 66. *KIAL*?= Kwa nini? . . . *ĈAR*= Kwa sababu, kwa kuwa, 49. — 67. Zoezi, 49.

Somo la nane51

68. Kikati cha udogo *-ET-*, 51. — 69. Kikati cha ukubwa *-EG-*, 51. — 70. Zoezi, 52. — 71. Kihusishi *DE*, 52. — 72. *DIRU AL MI*,= Uniambie., 53. — 73. Vionyeshi, 53. — 74. Neno *ĈI*, 54. — 75. Zoezi, 54. — 76. Virejeshi, 55. — 77. Zoezi., 56.

Somo la tisa.57

78. Kikati *-IST-*, 57. — 79. Zoezi, 58. — 80. Kikati *-IL-*, 58. — 81. *PER*= kwa, kwa njia ya., 58. — 82. Zoezi, 58. — 83. Zoezi, 59. — 84. Kikati *-AR-*, 59. — 85. Zoezi, 59. — 86. Vielezi vya wakati, 60. — 87. Zoezi, 61. — 88. Vielezi vingine, 61. — 89. Kiambishi tamati *-E*, 62. — 90. Zoezi, 62.

Somo la kumi63

91. Vielezi vingine vya mahali, 63. — 92. Zoezi, 63. — 93. Uundaji wa maneno, 64. — 94. Zoezi, 64. — 95. Kiambishi tamati *-U*, 64. — 96. Zoezi, 65. — 97. Vitenzi maalumu, 65. — 98. Neno *JEN*, 66. — 99. Misemo, 66. — 100. Majina ya heshima, 67. — 101. Maamkio, 67. — 102. Misemo mingine, 68. — 103. Vivumishi vingine, 68. — 104. Zoezi, 68. — 105. Zoezi., 69.

Viambishi vyote71

Kamusi75

Faharisi81

STRUKTURO DE LA ESPERANTO-MOVADO, 83.

Utangulizi

Madhumuni ya kitabu hiki ni kuwawezesha wale Waafrika wanaojua kusoma Kiswahili kujifunza lugha ya Kiesperanto bila mwalimu.

Litakuwa jambo la busara sana kwa wanafunzi kusoma kidogo kidogo kila siku, bila kusoma haraka kitabu kizima, na pia wao wafanye mazoezi yote katika kitabu hiki kwa kufuata mpango wa kitabu chenyewe. Katika kila zoezi kuna mfano unaowaonyesha wanafunzi namna ya kufanya zoezi lenyewe. Zaidi ya hayo wanafunzi watanufaika wakipeleka kazi zao kwa “UNIVERSALA ESPERANTO-ASOCIO”¹, ili mwalimu awaongoze kwa kuyasahihisha majibu yao. Anayejifunza akiyafuata masomo haya atafikia kiwango cha msingi cha ujuzi wa Kiesperanto. Kiwango cha upeo kitafikia kwa kufuata masomo ya kitabu kingine.

Maneno ya kisarufi yaliyomo katika kitabu hiki yanabainishwa katika KAMUSI YA KISWAHILI SANIFU, iliyotungwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na iliyochapishwa na Oxford University Press ya Dar es Salaam na Nairobi mnamo 1981, kwa hiyo litakuwa jambo la busara kujipatia kamusi hiyo, lakini katika kitabu hiki kila neno la kisarufi linabainishwa tena. Anayekuta shida yoyote tafadhali tuandikie barua.

Ĉi tiu lernolibro estas adapto de “Esperanto for beginners” verkita de M. C. Butler.

¹Tazama uk. 83

Mi tamen ne menciis la nomon de Butler sur la koverto por demeti de li ĉian respondecon pri la enhavo de ĉi tiu sŭahila versio. Fakte la de mi faritaj ŝanĝoj - ĉefe en la gramatikaj klarigoj - devontigas nur min porti la respondecon de ĉi tiu "Jifunze lugha ya Kiesperanto".

Batla estas ĉiakaze la metodo.

Prof. Nino Vessella

Latina (Italujo)

Somero 1982

nino@vessella.it

(Kvara revizio: 2020)

Somo la kwanza

1. Matamshi

Alfabeti: *A a, B b, C c, Ĉ ĉ, D d, E e, F f, G g, Ĝ ĝ, H h, Ĥ ĥ, I i, J j, Ĵ ĵ, K k, L l, M m, N n, O o, P p, R r, S s, Ŝ ŝ, T t, U u, Ŭ ŭ, V v, Z z.*

Irabu: *A a, E e, I i, O o, U u.*

Konsonanti: *B b, C c, Ĉ ĉ, D d, F f, G g, Ĝ ĝ, H h, Ĥ ĥ, J j, Ĵ ĵ, K k, L l, M m, N n, P p, R r, S s, Ŝ Ŝ, T t, Ŭ ŭ, V v, Z z.*

Irabu zote na konsonanti zifuatazo zinaonyesha sauti zile zile zinazoonyeshwa kwa herufi zile zile za Kiswahili:

B, D, F, G, H, K, L, M, N, P, R, S, T, V, Z.

Kwa hiyo, irabu zote na konsonanti zilizotajwa hutamkwa kama kwa Kiswahili.

Konsonanti zinazofuata zinaonyesha sauti zilizo katika Kiswahili, lakini kwa Kiswahili zinaonyeshwa kwa herufi tofauti:

Ĉ hutamkwa kama *CH* vile vile katika maneno mengi ya kiswahili: *chache, chama* n.k.

J (ambayo kwa kweli ni *kiyeyusho*) hutamkwa kama *Y*: *ndiyo, haya*, n.k.

Ŝ hutamkwa kama *SH*: *shaka, kwisha*, n.k.

Ŭ (ambayo kwa kweli ni *kiyeyusho*) hutamkwa kama *W*: *watu, Kiswahili, mwana*, n.k.

Konsonanti zifuatazo zinaonyesha sauti zisizopo katika lugha ya Kiswahili:

C hutamkwa kama TS katika neno la lugha ya Kiha *-otse* (maana yake *-ote*) na kama katika neno la lugha ya Kimunakiiya *buutsa* (*kuchukua*) na karibu kama TS katika neno la Kiingereza *cats* (*paka*);

\hat{G} hutamkwa kama J ya Kiswahili katika neno *njaa*, bila sauti ya n . Angalia pia kwamba sauti hiyo ni tofauti sana na sauti sahihi ya j katika neno *kuja* au ya neno *jina*. Hutamkwa pia kama DG katika neno la Kiingereza *porridge* (*uji*) na kama ج katika neno la Kiarabu *مَجْرِي* (*majira*) na hutamkwa kama J katika lugha ya Kigogo: *-inji* (*ingi*), lakini bila sauti ya N ;

\hat{H} hutamkwa kama X katika neno la lugha ya Kinyaturu *ukixaa* (*kukaa*) au kama خ katika neno la Kiarabu *مُخْتَصِر* (*muhtasari*);

\hat{J} hutamkwa kama S katika neno la Kiingereza *to measure* (*kupima*).

Je, unafahamu tofauti ya sauti za majozzi yafuatayo ya herufi?

$$\hat{c} \neq \hat{g} \quad \hat{s} \neq \hat{j} \quad l \neq r$$

2. Mkazo

Kiesperanto kinafanana na Kiswahili kuhusu mkazo. Irabu inayokazwa ni ile kabla ya irabu ya mwisho.

Kumbuka irabu ni: a, e, i, o, u tu!

3. Zoezi

Maneno ya orodha ya kushoto ni tofauti kabisa na maneno ya orodha ya kulia

<i>Ĝusta</i>	sawa, sahihi	<i>Justa</i>	-a haki
<i>Jako</i>	koti	<i>Ĵako</i>	plagi dume, aina ya kiunganisho cha umeme
<i>Ĵako</i>	plagi dume	<i>Ŝako</i>	sataranji
<i>tuŜi</i>	kagusa	<i>tuSi</i>	kukohoa
<i>Stelo</i>	nyota	<i>Ŝtelo</i>	wizi
<i>STelo</i>	nyota	<i>SITelo</i>	ndoo
<i>laSTa</i>	-a mwisho	<i>laSITa</i>	aliyeachwa
<i>aĴo</i>	kitu	<i>aĜo</i>	umri
<i>leĜo</i>	sheria	<i>leGo</i>	somo, usomaji
<i>Ĝelo</i>	namna ya mgando	<i>Ĉelo</i>	kijumba, seli
<i>peCo</i>	kipande	<i>peKo</i>	dhambi
<i>peCo</i>	kipande	<i>peZo</i>	uzito
<i>peCo</i>	kipande	<i>peSo</i>	uzani
<i>peSi</i>	kupima uzito, kuhesabu uzani	<i>peZi</i>	kuwa na uzito
<i>Horo</i>	saa	<i>Ĥoro</i>	kwaya
<i>Ĥoro</i>	kwaya	<i>Koro</i>	moyo
<i>koRo</i>	moyo	<i>koLo</i>	shingo
<i>iRo</i>	mwendo	<i>iLo</i>	ala
<i>biRdo</i>	ndege	<i>biLdo</i>	picha

<i>neeBLa</i>	siowezekana	<i>neBULa</i>	utusitisi / kwa moshi au kwa mvuke
<i>ŜVeli</i>	kuvimba	<i>ŜOVeli</i>	kupalilia kwa jembe

Zingatia matamshi sahihi ya maneno haya yenye mifuatano ya herufi ambayo lugha ya Kiswahili hairuhusu:

<i>lingvo</i>	lugha	<i>kvadrato</i>	mraba
<i>kompreni</i>	kufahamu	<i>frukto</i>	tunda
<i>kvalito</i>	jinsi, sifa	<i>semajno</i>	juma, wiki
<i>lipharoj</i>	msharubu	<i>stari</i>	kusimama
<i>montri</i>	kuonyesha	<i>proksima</i>	karibu
<i>kvadrato</i>	mraba	<i>ŝranko</i>	kabati
<i>skribi</i>	kuandika	<i>trudherbo</i>	gugu
<i>scii</i>	kujua	<i>fenestro</i>	dirisha
<i>edzo</i>	mume	<i>rajto</i>	haki, hoja
<i>ŝranko</i>	kabati	<i>ŝtrumpo</i>	soksi
<i>spicherboj</i>	viungo, majani ya kukolezea/kuungia chakula		

Somo la pili

4. Kibainishi

Kibainishi ni neno linaloleta dhana ya uhakika. Kwa Kiesperanto hutumika neno **la** ambalo huja kwanza katika fungu la maneno (yaani fungu la majina linayoyaletea “uhakika”). Matumizi ya neno hili yanaonyesha kitu (au vitu) fulani kili-chokwisha tambulishwa, au kinachojulikana:

Daresalamo estas urbo.

Dar es Salaam ni mji
(kama Nairobi, Kinshasa,
Maputo, ... n.k.)

La urbo estas bela.

Ule mji (uliotajwa, yaani:
Dar es Salaam, siyo mji
mwingine) ni mzuri.

Kwa Kiswahili inawezekana kubainisha uhakika wa kitu fulani kwa njia ya vionyeshi au vionyeshi (yaani: *ule, yule, kile,...* n.k.), lakini ni muhimu kutambua wazi kwamba dhana ya “uhakika” katika Kiswahili ni tofauti kidogo na dhana ya “uhakika” katika Kiesperanto.

Ni dhahiri kwamba ikiwa tunataja jina la pekee (kama *Juma, Nairobi, Luanda, Esperanto, Afrika, Kitaru, Abdallah*, n.k.) hatutumii kibainishi, kwa sababu jina la namna hiyo lina dhana ya uhakika ndani mwake mwenyewe.

5. Uundaji wa maneno

Kila neno la Kiesperanto huundwa kwa vipande vya usemi (au **mofimu**) mbali mbali vinavyowekwa pamoja kwa kufuata taratibu fulani maalumu. Kipande kinachobeba maana ya msingi katika maneno husika kinaitwa **mzizi**. Huu mzizi ndio kiini cha neno. Mzizi hauwezi kuchanguliwa tena katika sehemu nyingine bila kupoteza uamilifu wa utambulisho wake wa kimaana. Kipande cha pili kiitwacho **kiambishi tamati** ni mwisho wa neno unaoonyesha kazi za neno lenyewe katika sentensi na aina yake. Kipande cha mwisho ni **kiambishi awali** na viambishi vya ndani (viitwavyo vikati pia). Pengine itasaidia tukieleza kwamba “tamati” maana yake ni “mwisho, mwishoni”, “awali” maana yake ni “mwanzo, mwanzoni”:

neni: *jes* (ndiyo)

lina **mzizi:** *jes tu*

viambishi vimefichwa (tunasema kwamba ni
viambishi kapa)

neni: *bela* (-zuri)

lina **mzizi** (yaani: *bel-*) na

kiambishi tamati (yaani: *-a*)

neni: *malbela* (-baya)

lina **mzizi** (*bel-*),

kiambishi tamati (*-a*) na

kiambishi awali (*mal-*)

neni: *malbelela* (-baya kidogo)

lina **mzizi:** *bel-*

kiambishi awali: *mal-*

kiambishi cha ndani: *-et-*

kiambishi tamati: *-a*

neni: *malbelulino* (mwanamke asiye mzuri)

lina **mzizi:** *bel-*

kiambishi awali: *mal-*

kiambishi cha ndani: *-ul-*

kiambishi cha ndani: *-in-*

kiambishi tamati: -o

Mzizi kama ule wa *jes* (ndiyo) huitwa **mzizi-huru**, kwa sababu huweza kujitegemea wenyewe, yaani huweza kusimama peke yake kama neno kamili. Mzizi ambao hauwezi kujitegemea wenyewe huitwa **mzizi-funge**.

Matumizi ya viambishi hivi yanaleta mabadiliko ya maana, ya aina ya neno, na ya kazi ya neno katika sentensi. Mabadiliko yo yote yahitaji kila mara mabadiliko ya kiambishi:

-toto	<i>infan-</i>	-tu	<i>hom-</i>
mtoto	<i>infano</i>	mtu	<i>homo</i>
(m-toto)	<i>(infan-o)</i>		
watoto	<i>infanoj</i>	watu	<i>homoj</i>
kitoto,	<i>infane</i>	kimtu,	<i>home</i>
vitoto		vimtu	
utoto	<i>infaneco</i>	utu	<i>homeco</i>
kijitoto	<i>infaneto</i>	jitu	<i>homego</i>

6. Kiambishi -O

Kiambishi hiki cha mwisho hutumika kuonyesha jina (la kitu au la mtu, la mahali au la jambo, la matendo au la hali, au la kiumbe cho chote), yaani **nomino** zote :

<i>âambr-o</i>	<i>âambro</i>	chumba
<i>amik-o</i>	<i>amiko</i>	rafiki
<i>arb-o</i>	<i>arbo</i>	mti
<i>best-o</i>	<i>besto</i>	mnyama
<i>bild-o</i>	<i>bildo</i>	picha
<i>edz-o</i>	<i>edzo</i>	mume
<i>faden-o</i>	<i>fadeno</i>	uzi
<i>fil-o</i>	<i>filo</i>	mwana
<i>flor-o</i>	<i>floro</i>	ua (maua)
<i>frukt-o</i>	<i>frukto</i>	tunda

<i>hom-o</i>	<i>homo</i>	mtu
<i>infan-o</i>	<i>infano</i>	mtoto
<i>kaf-o</i>	<i>kafo</i>	kahawa
<i>konsil-o</i>	<i>konsilo</i>	shauri
<i>libr-o</i>	<i>libro</i>	kitabu
<i>lit-o</i>	<i>lito</i>	kitanda
<i>lok-o</i>	<i>loko</i>	mahali
<i>lun-o</i>	<i>luno</i>	mwezi
<i>mebl-o</i>	<i>meblo</i>	fenicha
<i>mur-o</i>	<i>muro</i>	ukuta
<i>orang-o</i>	<i>orangô</i>	chungwa
<i>patr-o</i>	<i>patro</i>	baba mzazi
<i>pord-o</i>	<i>pordo</i>	mlango
<i>roz-o</i>	<i>rozo</i>	waridi
<i>tabl-o</i>	<i>tablo</i>	meza
<i>tag-o</i>	<i>tago</i>	siku
<i>te-o</i>	<i>teo</i>	chai
<i>vir-o</i>	<i>viro</i>	mwanamume

7. Zoezi

Soma ukatafsiri kwa Kiswahili:

Kio estas tio? (Kile ni nini? Kile ni kitu gani?) **Tio** estas pordo. **Kio** estas kato (paka)? **Kato** estas besto. **Kio** estas tablo? **Tablo** estas meblo. **Kio** estas orangô? **Orangô** estas frukto. **Kio** estas rozo? **Rozo** estas floro.

(Jina unalotumia kwa kujibu neno **kio** lazima liwe na kiambishi tamati **o**).

8. Kiambishi -A

Kiambishi tamati hiki hutumika kuonyesha neno linalosifu jina (au *nomino*) au huonyesha aina ya mtu au ya kitu fulani. Neno lenye kiambishi tamati hicho huitwa “kivumishi cha sifa” au

kivumishi tu. Kwa Kiswahili maneno mengi yaliyoonyesha sifa ya jina hayapatanishi ngeli ya jina yanalolisifu, bali kwa Kiesperanto kila neno linaweza kufanya kazi ya kivumishi kwa kubadilika tu kiambishi tamati.

mtu mrefu (urefu wa kwenda juu)	<i>alt-A</i>	<i>alta homo</i>
mtu wa saburi	<i>pacienc-A</i>	<i>pacienca homo</i>
mtu mwenye mali, tajiri	<i>riĉ-A</i>	<i>riĉa homo</i>

Hebu chunguza mafungu yafuatayo hapa chini

yule mtu ni mrefu	<i>la homo estas alta</i>
bilauri iliyojaa	<i>plena glaso</i>
ile bilauri ² iliyojaa	<i>la plena glaso</i>
ile bilauri imejaa	<i>la glaso estas plena</i>

darasa kubwa	<i>granda klaso</i>
lile darasa kubwa	<i>la granda klaso</i>
lile darasa ni kubwa	<i>la klaso estas granda</i>

Ujifunze vivumishi vya hapa chini

<i>bela</i>	-zuri	<i>bona</i>	-ema
<i>dika</i>	-nene	<i>forta</i>	-enye nguvu, kali, imara
<i>granda</i>	-kubwa	<i>kontenta</i>	-radhi, -furahifu
<i>longa</i>	-refu (urefu wa kwenda mbele, au wa muda)	<i>mola</i>	-ororo, -tefu, laini
<i>nova</i>	-pya	<i>pura</i>	safi
<i>sana</i>	-zima, -enye afya	<i>varma</i>	-enye joto, -a moto
<i>vera</i>	-a kweli	<i>verda</i>	-enye rangi ya kijani

²Siku hizi ni *glasi*!

9. Zoezi

Andika sentensi kwa kutumia maneno **la** na **estas** kama mfano ufuatao:

Alta tablo (meza ndefu) **La** alta tablo.
La tablo estas **alta**!

Endelea:

Bela floro. *Bona* konsilo. *Dika* muro. *Forta* viro. *Granda* bildo. *Kara* (mpendwa) patro. *Longa* tago. *Mola* lito. *Nova* luno. *Pura* loko. *Sana* homo. *Verda* libro. *Longa* fadeno. *Vera* amiko. *Alta* arbo.

Sasa tafsiri sentensi ulizoziandika.

10. Maneno machache

Angalia matamshi ya mifuatano ya herufi katika maneno haya:

<i>krajono</i>	kalamu, pensili	<i>fenestro</i>	dirisha
<i>glaso</i>	bilauri, gilasi	<i>klaso</i>	darasa
<i>pupitro</i>	meza, deski	<i>lernanto</i>	mwanafunzi
<i>instruisto</i>	mwalimu	<i>kreto</i>	chaki
<i>frukto</i>	tunda	<i>stelo</i>	nyota
<i>bildo</i>	picha	<i>birdo</i>	ndege
<i>plafono</i>	dari, sakafu ya juu	<i>objekto</i>	kitu
<i>frato</i>	kaka, ndugu (wa mzazi mmoja)	<i>plumo</i>	unyoya, kalamu ya wino

11. Zoezi

Chunguza sentensi zifuatazo:

Kia estas la *fadeno*? Ule uzi ni wa namna gani?

La fadeno estas longa. Ule uzi ni mrefu.

Sasa jibu maswali yafuatayo kwa kutumia neno lenye kiambishi tamati ***a***:

Kia estas la *pordo*? ***Kia*** estas la *plafono*? ***Kia*** estas la *plumo*? ***Kia*** estas la *bildo*? ***Kia*** estas la *tago*? ***Kia*** estas la *krajono*? ***Kia*** estas la *kafo*? ***Kia*** estas la *lito*? ***Kia*** estas la *floro*? ***Kia*** estas la *teo*?

Somo la tatu

12. Kiambishi awali *MAL-*

Kiambishi hiki kinafanya kazi sawasawa ya irabu *-u-* katika maneno yafuatayo toka Kiswahili:

kufunga	(<i>fermi</i>)	kufung- u -a	(<i>mal-fermi</i>)
kuficha	(<i>kaŝi</i>)	kufich- u -a	(<i>mal-kaŝi</i>)

yaani kiambishi hiki huyageuza maneno ili kuonyesha kinyume cha maneno yenyewe. Angalia kwamba kiambishi hicho hutumika kwa maneno ya aina yoyote kwa Kiesperanto:

<i>juna</i>	-changa	<i>mal-juna</i>	-zee, -a kizee
<i>ordo</i>	utaratibu	<i>mal-ordo</i>	<i>fujo</i>
<i>amo</i>	mapenzi, upendo	<i>mal-amo</i>	<i>chuki</i>
<i>luma</i>	-enye nuru, -angavu	<i>mal-luma</i>	-a giza, -eusi

Basi, kinyume cha maneno mengine ulijojifunza mpaka sasa ni:

<i>maldika</i>	-embamba	<i>malgranda</i>	-dogo
<i>mallonga</i>	-fupi (kwa kwenda mbele)	<i>malplena</i>	-tupu
<i>malsana</i>	-gonjwa	na kadhalika...	

Mifano:

<i>mola pano</i>	mkate	<i>malmola pano</i>	mkate
	mororo		mkavu
<i>pura akvo</i>	maji safi	<i>malpura akvo</i>	maji
			machafu
<i>bona knabo</i>	mvulana	<i>malbona</i>	mwanafunzi
	mwema	<i>lernanto</i>	mbaya

13. Zoezi

Soma ukatafsiri kwa Kiswahili:

Malalta plafono. Malbela viro. Malbona banano (ndizi).
Maldika glaso. Malforta fadeno. Malgranda filo. Mallonga krajono. Malnova kajero (daftari). *Malplena glaso. Malpura objekto. Malsana frato. Malvarma loko. Malbela libro. Maljuna hundo* (mbwa). *Malkontenta kato* (paka).

14. Kiambishi -J

Kiambishi hiki ni kiwakilishi cha wingi.

Kwa Kiswahili mabadiliko ya jumla yahitaji mabadiliko ya ngeli ya jina: *mtu mmoja* (jumla ya umoja), *watu wengi* (jumla ya wengi/wingi).

<i>boto</i>	buti (kiatu kirefu)	<i>boto-j</i>	ma -boti
<i>mano</i>	mkono	<i>mano-j</i>	mi -kono
<i>patro</i>	baba	<i>patro-j</i>	ma -baba
<i>tempo</i>	wakati	<i>tempo-j</i>	ny -akati
<i>viro</i>	mwanamume	<i>viro-j</i>	wa -naume

Maneno ya ngeli moja kwa Kiswahili hayabadiliki. Hata maneno hayo kwa Kiesperanto yanatakiwa yawe na kiambishi cha wingi. Kwa mfano

lando nchi *landoj* nchi

15. Zoezi

Rudia maneno ya vifungu vya 6 na 10 katika wingi kama mfano ufuatao:

(Amiko) Amikoj. Marafiki.

16. Mifuatano ya maneno -AJ -OJ

Kiambishi cha wingi *j* hutumika pia mwishoni pa vivumishi katika vikundi kama hivi:

la ruĝaj libroj **vile vitabu vyekundu**

basi katika umoja tunavyo viambishi *-a -o* lakini katika wingi tunayo mifuatano ya viambishi *-aj -oj*, kwa sababu ya upatanishi wa kisarufi.

ANGALIA! Kibainishi hakichukui kiambishi cha wingi.

17. Mfululizo wa vivumishi

Kwa utokezo wa mazoeza vivumishi hutangulia jina vinalolisifu: vile vitabu vipya vyekundu kumi

La dek novaj ruĝaj libroj
Kumi vipya vyekundu vitabu

lakini hakuna sheria hasa juu ya upangaji wa sifa hizi za mchanganyiko katika sentensi.

18. Zoezi

Rudia vifungu vya 9 na 13 katika wingi kama mfano ufuatao:

Altaj tabloj

La malbelaj viroj

Meza ndefu

Wale wanaume wasio wazuri

19. Kumbuka!

Wingi wa vitu (au jina lolote) huonyeshwa kwa kuweka kiambishi *j* mwishoni pa jina na pa kivumishi cha sifa (kikiwapo), lakini siyo mwishoni pa “kibainishi” *la*.

20. Neno *ESTAS*

Estas ni kitenzi; maana yake: *ni* au *yu* au *u* au *m* au *wa* n.k.):

Mifano:

La tasko estas simpla.

La taskoj estas simplaj.

La vortoj estas longaj.

La forkaj estas akraj.

La plankoj estas lignaj.

La benkoj estas malnovaj.

Kazi ile **ni** rahisi.

Kazi zile **ni** rahisi.

Maneno yale **ni** marefu.

Nyuma zile **ni/zi** kali.

Sakafu zile **ni/zi** za miti.

Viti vile **ni/vi** vichakavu.

ANGALIA! Mara nyingi kwa Kiswahili haitakiwi kitenzi *kuwa* (yaani maneno *ni*, *yu*, *ki*, *u*, *m*, n.k.): ukisema *Juma mfalme*, *Asha mwanamke*, neno lile “*ni*” au “*yu*”, n.k., linafichika (yaani limo katika fikira zako tu).

Kwa Kiesperanto lazima utie kila mara neno hilo kati ya maneno mawili haya ya sentensi zilizoonyeshwa, yaani:

Ĝumo estas reĝo.

Aŝa estas virino.

Juma mfalme.

Asha mwanamke.

21. Jifunze maneno yafuatayo

<i>kaj</i>	na
<i>sed</i>	lakini, bali
<i>ne estas</i>	si
<i>de</i>	-a (yaani: cha, vya, mwa, wa, ya, n.k.)
<i>en</i>	katika, ndani ya, -ni: -ni <i>Estas kafo en la taso.</i> Mna kahawa kikombeni mle.
<i>sur</i>	juu ya, -ni: -ni <i>La libro de Ĉilongo estas sur la tablo.</i> Kitabu cha Chilongo kipo mezani pale.

22. Zoezi

Tafsiri kwa Kiswahili ukilingana na mfano:

Mfano: *La nomo de la viro estas Ernesto.*
Jina la yule mwanamume ni Ernesto.

La floro estas freŝa (-bichi, -changa). *La pano ne estas freŝa* (-pya, -tefu, uliopo). *La ŝafo* (kondoo) *ne estas granda*. *La ŝafoj ne estas grandaj*. *En la libro estas bildo* (picha). *En la libro estas bildoj*. *La libro de la knabo estas sur la planko*. *La fiŝo* (samaki) *estas en la akvo*. *La viroj estas en la ŝipo* (meli). *La libro kaj la plumo estas* (vipo) *sur la tablo*. *La patro estas bona, sed la frato estas malbona*.

23. Zoezi

Jibu maswali haya kwa kutumia sentensi za kifungu cha 22. Baadaye tafsiri.

Kio estas sur la tablo? Kio estas en la libro? Kio estas sur la planko? Kio estas en la ŝipo ?

Kie = wapi? *Tie* = pale, kule, mle.

Kie estas la libro de la knabo? La libro de la knabo estas tie sur la planko.

Kie estas la fiŝo? Kie estas bildoj? Kie estas la libro kaj la plumo? Kie estas la viroj?

Kia estas la floro? Kia estas la ŝafo? Kia estas la pano? Kia estas la patro?

Je, ulitumia pia kiambishi awali *mal* katika majibu yako?

Somo la nne

24. Kitenzi

Kitenzi kinaonyeshwa kwa kiambishi cha mwishoni *-i* kina-
chofanya kazi ile ile ya kiambishi awali cha Kiswahili *ku-*:

<i>danc-i</i>	ku cheza dansi	<i>leg-i</i>	ku soma
<i>dorm-i</i>	ku lala (usingizi)	<i>lud-i</i>	ku cheza
<i>est-i</i>	ku wa	<i>plor-i</i>	ku lia (machozi)
<i>kant-i</i>	ku imba	<i>rid-i</i>	ku cheka
<i>kur-i</i>	ku kimbia	<i>sid-i</i>	ku kaa, ku keti
<i>kuŝ-i</i>	ku lala (chini)	<i>skrib-i</i>	ku andika
<i>labor-i</i>	ku fanya kazi	<i>star-i</i>	ku simama

Lakini angalia kwamba unapotumia neno la kitenzi lenye
kiambishi awali **ku-** ili kuonyesha kitenzi kinapofanya kazi ya
nomino peke yake, kwa Kiesperanto hutumika neno lenye ki-
ambishi cha mwishoni *-O*:

Kuimba **kwa** Juma ni **ku**baya. *La kanto de Ĝumo estas
malbela.*

25. Kiambishi tamati *-AS*

Kiambishi tamati hicho ni kiwakilishi cha njeo ya wakati, yaani
kinaonyesha kwamba tendo latendeka wakati huu wa sasa,

wakati uliopo, au kwa kawaida.

Nikisema *La pano estas sur la tablo*, ninafikiri wakati huu huu wa sasa. Angalia pia kwamba nikisema kwa Kiswahili “nimelala” ninamaanisha wakati huu wa sasa, yaani nilianza kulala kabla ya sasa hivi lakini bado niko kitandani, kwa Kiesperanto tunatumia tena kiambishi tamati **-AS**. Hata nikisema kwa Kiswahili “yeye hulala” au “yeye alala”, kwa Kiesperanto ninatumia tena kiambishi tamati **-AS**.

Kwa hiyo:

Li dormas =Analala, Alala, Hulala, Amelala

Li staras =Anasimama, Asimama, Husimama, Amesimama

26. Mtendaji

Mifano ya kifungu cha 25 yakuonyesha kwamba kwa Kiesperanto havitumiki viwakilishi vya mtendaji (au viambishi vya nafsi) kama

a- (*alala, analala, amelala =Li dormas*),

bali hutumika neno la *li*, yaani lazima kutaja kila mara jina lenyewe la mtendaji (kiima) au badala yake maneno ya hapa chini yanayoitwa **viwakilishi (vya) nafsi**:

MI	mimi, ni-, n-, si-
VI	wewe, u-, w-, hu-
LI	yeye, a-, yu-, n.k. (kwa wanaume tu)
ŜI	yeye, a-, yu-, n.k. (kwa wanawake tu)
ĜI	yeye, ki-, i-, n.k. (kwa vitu na wanyama)
NI	sisi, tu-, tw-, hatu-
VI	ninyi, m-, mw-, ham-, hamw-
ILI	wao, wa-, vi-, zi-, n.k.

27. Zoezi

Tafsiri kwa Kiswahili:

*Mi sidas kaj skribas. Li kuŝas kaj ripozas (kupumzika).
Ni staras kaj legas. Ŝi estas en la ĉambro. Kie ĝi dormas?
Mi sidas. La hundoj kuras. La birdoj flugas (-ruka). La kato
kuŝas sur la lito. La knabo dormas en la lito.*

28. Zoezi

Angalia mifano ifuatayo:

Swali: **Kiu** estas vi? Wewe ni nani?

Jibu: *Mi estas Aŝa.* Mimi ni Asha.

Tafsiri kwa Kiswahili:

Kiu kantas? *Ŝi kantas.*

Kiu estas malbona knabo? *Li.*

Kiu parolas (-ongea, -zungumza)? *Vi.*

29. Neno NE

Neno hilo ndilo la kukataa au kukanusha. Kiswahili hubainisha uyakinishi na ukanushi kama ifuatavyo:

Uyakinishi

Mwalimu anasimama

Walimu wanasimama

Ninasoma

Anafanya kazi

Ukanishi

Mwalimu **hasimami**.

Walimu **hawasimami**.

Sisomi;

Hafanyi kazi;

kwa Kiesperanto lazima tutumie neno la kukanusha **ne** mara moja kabla ya jina la matendo (au jina lolote la kukanushia). Angalia katika sentensi zifuatazo jinsi neno la kukanusha linavyotumika:

Mwalimu **hasimami**.

Walimu **hawasimami**.

Moyo ule **haupigi**.

Mioyo ile **haipigi**.

*Instruisto **ne** staras.*

*Instruistoj **ne** staras.*

*La koro **ne** batas.*

*La koroj **ne** batas.*

Chakula **hakitoshi**.

Vyakula **havitoshi**.

n.k.

Manĝaĵo **ne** *sufiĉas*.

Manĝaĵoj **ne** *sufiĉas*.

k.t.p. (*kaj tiel plu*)

30. Zoezi

Tafsiri kwa Kiswahili:

La pano ne sufiĉas. Ĝi ne estas freŝa. Ŝi ne estas bela, sed ŝi ne estas malbela. Ili ne ploras, ili ridas. Vi ne laboras, vi ludas. Ni ne staras sur la benko, ni sidas sur ĝi.

31. Vihusishi

Kwa Kiswahili maongezo ya maana ya sentensi inawezekana kupatikana kwa kubadili mwisho wa kitenzi (hasa kwa kiambishi nyambulishi cha kitendea) au kwa kutumia maneno kama **kwa, na, kwa ajili ya, kabla ya, baada ya, karibu na, juu ya, chini ya**, n.k. maneno haya yaitwa kwa Kiesperanto **prepozicioj** na katika sarufi hii tutayaita **vihusishi** kwa Kiswahili. Kihusishi ni aina moja ya viunganishi.

32. **APUD** = karibu na

Tafsiri kwa Kiswahili:

*La teo estas **apud** la kafo. La hundo dormas **apud** la fenestro. Li sidas **apud** ŝi. La lito staras **apud** la muro.*

33. **SUB** = chini ya, -ni

Tafsiri kwa Kiswahili:

*Ili sidas **sub** la suno. La planko estas **sub** la plafono. La skatolo (mkebe) estas **sub** la tablo.*

34. AL

Al huwa inaonyesha jinsi ya kufanyia tendo lenyewe lilivyo. Kwa kusema kweli mara nyingi vitenzi vya kufanyia haiwezekani kuvitafsiri kwa kutumia kihusishi **al**. Chunguza sentensi zifuatazo:

Nin ak utakia...	<i>Mi deziras al vi...</i>
Tun aw asomea.	<i>Ni legas al ili.</i>
Un am wongea	<i>Al kiu vi parolas?</i>
Nin ak wenda sokoni.	<i>Mi iras al bazaro.</i>
Amet ule tea machungwa.	<i>Li portis oranĝojn al ni.</i>

LAKINI

Un am zungumzi a nani?	<i>Pri kiu vi parolas?</i>
Amet un unuli a machungwa.	<i>Li aĉetis oranĝojn por ni.</i>
U tu ombe e !	<i>Preĝu por ni!</i>

Tunaweza kusema kwamba vitenzi vinayyoishia na **-ea** au **-ia** mara nyingi kwa Kiesperanto vinafuatwa na *prepozicioj* (vihusishi).

35. Zoezi

Tafsiri kwa Kiswahili:

Ili kuras al ni. Ŝi kantas al li, sed li ne kantas al ŝi. La hundoj kuras al la knabo. La birdoj flugas al la arbo.

Somo la tano

36. Maswali

Umejifunza viulizi vinne ambavyo hutumika kuulizia swali:

KIA? (-a aina gani?) hutumika kwa kuuliza kuhusu sifa, kwa hiyo jibu lazima liwe na kivumishi, yaani neno lenye kiambishi tamati **-A**

Swali **KIA?** Jibu: **-A**

Mfano: **KIA** *estas la floro?* *La floro estas bela.*

KIO? (nini?) hutumika kwa kuuliza kuhusu kitu au kazi ya watu,, kwa hiyo jibu lazima liwe na nomino, yaani neno lenye kiambishi tamati **-O**

Swali **KIO?** Jibu: **-O**

Mfano: **KIO** *estas bela?* *La floro estas bela.*

KIE? (-pi?) hutumika kwa kuuliza kuhusu mahali (wapi? mahali gani?)

KIU? hutumika kwa kuuliza kuhusu mtu (nani?) au kama **-pi** katika sentensi kama zifuatazo:

Kalamu **ipi** ni yako?

KIU *plumo estas (la) via?*

Neno jingine **Ĉu** pia hutumika kuulizia swali, bali neno hutumika kama jibu itakuwa “Ndiyo!” (**Jes!**) au “Hapana!” (**Ne!**)

(Mara kwa mara kwa Kiswahili pia hutumika kiulizi kama **ĉu**, yaani **je.**)

Je, unakuja? Ndiyo, nakuja. **Ĉu** vi venas? *Jes, mi venas*

Angalia kama viulizi vya Kiesperanto hutumika mwanzoni kabisa mwa maswali, bali viulizi vya Kiswahili hutumika mwishoni:

Kion vi portis al mi?

Umeniletea **nini**?

lakini, pia:

Kiu rompis ĉi tiun plumon?

Nani aliyeivunja kalamu hii?

Kiu plumo estas (la) via?

Kalamu **ipi** ni yako?

ANGALIA pia kwamba kwa Kiesperanto sentensi bila kiulizi chochote siyo kabisa swali:

La bano estas preta.

Maji ya kuoga ni tayari.

Ĉu la bano estas preta?

(Je,) Maji ya kuoga ni/yako tayari?

Inawezekana kujibu:

Jes, ĝi estas preta.

Ndiyo, (yako) tayari.

au

Ne, ĝi ne estas preta.

Hapana. Si tayari.

hiyo ndiyo sababu ikawa *si swali* sentensi “*La hundo kuras?*”, kwa hivyo yafaa ujikumbushe kutumia kila mara kielezi **Ĉu** au vielezi vyenye herufi **K**- mwanzoni mwa swali!

37. Zoezi

Ukiulizwa:

Ĉu li dancas? Je, anacheza dansi?

unaweza kujibu:

Jes, li dancas. Ndiyo, anacheza dansi.

au:

Ne, li ne dancas. Hapana, hachezi dansi.

Pia swali:

Ĉu la birdoj kantas? Je, wale ndege wanaimba?

linataka jibu:

Jes, ili kantas. Ndiyo, wanaimba.

au:

Ne, ili ne kantas. Hapana, hawaimbi.

Sasa jibu wewe mwenyewe, halafu tafsiri maswali na jibu:
*Ĉu la nokto (usiku) estas longa ? Ĉu la kuzoj (mtoto mwana-
mume wa ndugu wa mzazi mmoja; binamu) estas junaj?*

38. Misemo akali

Jifunze majibu haya yafuatayo:

Ĉu mi estas prava?

Nina haki?

au: Nimesema kweli?

au: Nimesema vizuri?

MAJIBU:

Jes. Komprenoble vi estas.

Ndiyo. Bila shaka.

Komprenoble ne.

Hasa siyo. Hakika siyo.

Eble jes.

Pengine ndiyo. Huenda ndiyo.

Eble ne.

Labda siyo.

Efektive, vi estas malprava.

Kwa kusema kweli umekosea.

39. Misemo mingine

Jifunze majibu haya mengine:

Ĉu li estas tie?

Yuko? Yupo? Yumo?

MAJIBU:

Eble jes.

Labda yuko.

Kompreneble ne.

Hasha, hayuko.

Se jes, li...

Kama yuko, a-.....

Se ne, li ...

Kama hayuko, a-.....

40. Maswali

Jifunze namna ifuatayo ya kuuliza:

Li estas tie, ĉu ne?

Yupo au sivyo?

Li ne estas tie, ĉu?

Hayupo au sivyo?

Yafaa ukumbuke kwamba neno **ne** likitumikwa katika sentensi yenyewe, mara nyingi neno hilo halitakiwi mwishoni.

41. Zoezi

Tafsiri:

Kiu legas? La kuzo legas. - Al kiu li legas? Li legas al mi. - Kia li estas. Li estas bona. - Kie li estas? Li estas en la ĉambro. - Kio li estas? Li estas lernanto. - Kio estas tio? Ĝi estas nur (tu) libro. - Kia estas la libro? Ĝi estas granda. - Kie ĝi estas? Ĝi estas sur la tablo. - Ĉu la vojo (njia) estas longa? Ne, ĝi ne estas longa: ĝi estas tre (sana) mallonga.

Tafsiri kwa Kiesperanto:

Yupi amekuja?- Ulisema miti imeanguka; ipi? - Unataka mche; nikupe upi? - Nimwadhibu yupi?

42. Kiambishi tamati **-IS**

Umeshasoma kwamba maneno yanayoonyesha tendo lile latendeka wakati huu wa sasa, wakati uliopo au kwa kawaida yana kiambishi tamati **-as**. Ili kuonyesha wakati uliopita wa kitenzi Kiswahili kinatumia kiambishi **-li-**, Kiesperanto kinatumia kiambishi tamati **-is**:

<i>mi estis</i>	nilikuwa	<i>mi ripozis</i>	nilipumzika
<i>mi laboris</i>	nilifanya kazi	<i>mi venis</i>	nilikuja
<i>mi ludis</i>	nilicheza	<i>mi vokis</i>	niliita

La infano ludis.

Yule mtoto alicheza

La viroj laboris.

Wale wanaume walifanya kazi.

Li estis tie, ĉu ne?

Alikuwa pale, sivyo?

Ĉu li venis?

Je, alikuja?

Ĉu vi ripozis?

Je, ulipumzika?

43. Zoezi

Rudia sentensi za vifungu vya 27, 28 na 30 ukitumia alama ya wakati uliopita badala ya kila alama ya wakati uliopo, halafu tafsiri sentensi hizo mpya.

Kwa mfano:

Mi sidas kaj skribas.

Ninakaa na ninaandika.

Mi sidis kaj skribis.

Nilikaa na niliandika. Nilikaa nikaandika.

44. Kikati **-IN-**

Kiambishi hicho hutwa katikati ya maneno yenyewe ili kuonyesha kwamba maneno hayo yanahusu watu au wanyama wa kike, kwa hiyo *patro* ni “baba mzazi”, *patrino* ni “mama mzazi”!

<i>Bovo</i>	ng'ombe dume	<i>Bovino</i>	ng'ombe jike
<i>Ĉevalo</i>	farasi dume	<i>Ĉevalino</i>	farasi jike
<i>Reĝo</i>	ufalme	<i>Reĝino</i>	malkia

45. Zoezi

Tunga sentensi kulingana na mfano huu:

avo kaj avino =babu kwa nyanya

ukitumia maneno yafuatayo:

filo, frato, kato, knabo, kuzo, lernanto, amiko, patro, onklo
(ami, mjomba, baba mdogo, baba mkubwa), *ŝafo* (kondoo),
viro, edzo.

Somo la sita

46. Rangi

<i>blanka</i>	-eupe	<i>lazura</i>	-a samawi
<i>blua</i>	-a buluu	<i>nigra</i>	-eusi
<i>bruna</i>	-a kahawa	<i>oranĝa</i>	-a manjano mabivu
<i>flava</i>	-a manjano	<i>ruĝa</i>	-ekundu
<i>griza</i>	-a kijivu, -a jivu	<i>verda</i>	-a kijani, -a majani

Tumia maneno haya hapa juu ukitunga sentensi kumi kama mfano ufuatao:

Kia estas la koloro de banano?

Banano estas flava.

47. Nambari

Ujifunze kuhesabu kwa Kiesperanto:

1	<i>unu</i>	2	<i>du</i>	3	<i>tri</i>	4	<i>kvar</i>	5	<i>kvin</i>
6	<i>ses</i>	7	<i>sep</i>	8	<i>ok</i>	9	<i>naŭ</i>	10	<i>dek</i>

Ukitaka kuendelea kwa Kiswahili unatumia neno **na** namba kumi na namba moja mpaka tisa: kumi **na** moja... kumi **na** tisa. Kwa Kiesperanto halitumika neno lolote:

11	<i>dek unu</i>	12	<i>dek du</i>
13	<i>dek tri</i>	... 19	<i>dek naŭ</i>

Sasa angalia. Namba ishirini ni “kumi mara mbili” au “mbili mara kumi” ($2 \times 10 = 20$), kwa hiyo kwa Kiesperanto ni: $2(x)10 = 20$ yaani *du-dek = dudek*.

Tukiendelea tunapata:

20 <i>dudek</i>	30 <i>tridek</i>	... 90 <i>naŭdek</i>
21 <i>dudek unu</i>	32 <i>tridek du</i>	... 99 <i>naŭdek naŭ</i>

100 *cent*

101 *cent unu* 111 *cent dek unu* 122 *cent dudek du* 133 *cent tridek tri* ...

999 *naŭcent naŭdek naŭ*

1000 *mil*

1001 *mil unu* ... 1011 *mil dek unu* ... 1111 *mil cent dek unu* ...

2000 (2×1000) *dumil*... n.k. *k.t.p.*

48. Upangaji wa kivumishi

Angalia kwamba upangaji wa kivumishi cha sifa ya kuhesabia ni tofauti kabisa na ule wa Kiswahili: kivumishi hicho hutajwa kabla ya jina lenyewe:

Du birdoj en unu kaĝo.

Ndege wawili ndani ya kitundu kimoja.

Ukitaka kueleza jina moja kwa kutumia vivumishi viwili au zaidi, upangaji wa vivumishi vya mchanganyiko huo ni karibu kinyume cha upangaji wa Kiswahili. Soma tena kifungu cha 17.

49. Zoezi

Tafsiri:

La tri knabinoj ludis en la ĝardeno (bustani). Sur la seĝo (kiti) estis kvar libroj kaj du plumoj. Ses aŭ sep glasoj estas sur la tablo. En la strato (nĵia) estas ducent domoj (nyumba). La domo staras inter (katikati ya) du arboj.

50. Zoezi

Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno na nombari za mwishoni. Fanya kama mfano:

Sur la tablo estas ... (5/libroj).

MFANO: *Sur la tablo estas kvin libroj.*

En la ĉambro estas ... (3/virinoj).

En la klas-ĉambro sidas ... (16/infanoj).

Sur la breto (rafu) estas ... (7/vazoj).

Sasa tafsiri sentensi zote ulizozikamilisha na sentensi zifuatazo:

En unu jaro (mwaka) estas dek du monatoj (miezi). Kiu numero venas post (hufuata) ses? Kiu numero venas antaŭ (hutangulia) dek tri? Kiu numero venas inter sep kaj naŭ?

Angalia mahesabu yafuatayo. Je unaweza kutafsiri kwa Kiswahili?

$2 + 3 = 5$ Du **kaj** tri estas kvin.

AU: Du **plus** tri estas kvin.

$5 - 2 = 3$ Kvin **minus** du estas tri.

$6 : 2 = 3$ Ses **one** je du estas tri.

AU: Du**one** ses estas tri.

AU: Ses du**one** estas tri.

$4 \times 7 = 28$ Kvar**oble** je sep estas dudekok.

AU: Sep**oble** kvar estas dudek ok.

AU: Kvar sep**oble** estas dudek ok.

-on- na -obl- na -e ni viambishi vingine.

51. Viulizi

Kiom? -ngapi? (bila jina)
Kiom da ...oj? -ngapi? Kiasi gani cha ... ?
-ngapi -a ...? (kinafuatwa na jina)

Chunguza mifano ifuatayo:

Kiom estas 2 plus 2? Mbili kuzidisha mbili ndio ngapi?

Kiom da mono pagis Daudi? Daudi alilipa kiasi gani cha fedha?

Kiom da mangoj li kolektis sub tiu arbo? Aliokota maembe mangapi chini ya mti ule?

Jibu kwa Kiesperanto:

Kiom estas 5 + 6? ***Kiom estas 4 + 9?*** ***Kiom estas 16 - 8?*** ***Kiom estas 4 x 9?*** ***Kiom estas 15: 5?*** sasa jibu ukitumia sentensi za kifungu cha 50.

Kiom da libroj estas sur la tablo? ***Kiom da virinoj estas en la cambro?*** ***Kiom da vazoj estas sur la breto?*** ***Kiom da infanoj sidas en la klasambro?*** ***Kiom da monatoj estas en unu jaro?***

52. Mtendaji na mtendewa

Katika sentensi

“anaona” ile **a**

ya mwanzoni yaonyesha anayefanya tendo, yaani **kiima**. Tume-shaona kwamba kwa Kiesperanto badala ya kile kiambishi cha nafsi cha mtendaji (k.m. ile **a** katika **anaona**) hutumika ki-wakilishi cha nafsi au jina lenyewe la mtendaji:

Ŝi vidas

Miriamo vidas

Anaona

Miriam anaona

ile *Ŝi* ni kiwakilishi cha mtendaji.

Zaidi ya hayo, mara nyingi neno la tendo, yaani kitenzi, katika Kiswahili huwa na sehemu nyingine inayoonyesha mtu au kitu kinachotendewa kitendo chenyewe, yaani kiambishi cha nafsi ya mtendewa au **yambwa**. Alama hii hutiwa katikati ya kitenzi chenyewe na huitika kikati cha mtendewa:

Ile

wa katika **anawaona**

yaonyesha mtendewa huyo.

Kwa Kiesperanto hutumika kiambishi tamati **-n** mwishoni pa kiwakilishi au mwishoni pa jina lenyewe la mtendewa:

Ŝi vidas ilin Anawaona

Angalia kwamba mara nyingi, hasa kwa jinsi ya kufanyia, **kutendea** matumizi ya alama za mtendewa yanatofautiana sana katika lugha hizo mbili (rudia pia kifungu cha 34):

Mi amas.

Mi amas vin.

Mi skribas.

Mi skribas al vi.

Mi skribas leteron al vi.

Ninapenda.

Ninakupenda.

Ninaandika.

Ninakuandikia.

Ninakuandikia barua.

Angalia kwamba alama ya mtendewa hutumika pia mwishoni pa viulizi hivi: **kia, kie, kio, kiu**.

Matumizi halisi ya alama hiyo utajifunza utakaposoma sarufi nyingine, kwa sasa chunguza mifano ifuatayo:

Ŝi vidas.

Kiu vidas? Ŝi.

Ŝi vidas arbon.

Kion ŝi vidas? Arbon.

Li vokas.

Kiu vokas? Li.

Anaona.

Nani ana(ye)ona? Yeye.

Anaona mti.

Anaona nini? Mti.

Anaita.

Nani ana(ye)ita? Yeye.

Li vokas ŝin.

Anamwita.

Kiun li vokas? Ŝin.

Anamwita **huyu**.

Mi dankas vin.

Ninaku**shukuru**.

Li vidas ilin.

Ana**wa**ona.

*Mi donas **al** vi ...*

Ninaku**p**a ...

53. Zoezi

Tafsiri.

Mi amas vin. La infano amas ĉokoladon (chakleti). La patrino legas libron. La patro skribas leteron. La infano ludas futbalon (mchezo wa mpira wa miguu). La instruisto amas la lernantojn.

54. Vitenzi akali

Ujifunze maneno yafuatayo:

<i>aĉeti</i>	kununua	<i>lerni</i>	kujifunza	<i>trinki</i>	kunywa
<i>aŭdi</i>	kusikia	<i>manĝi</i>	kula	<i>tuŝi</i>	kugusa
<i>havi</i>	kuwa na	<i>puni</i>	kuadhibu	<i>vendi</i>	kuuza
<i>helpi</i>	kusaidia	<i>rompi</i>	kuvunja	<i>viŝi</i>	kufuta

55. Zoezi

Tafsiri:

Ĉu vi amas min? Kion vi havas en la mano? Ĉu vi vendis dek bananojn aŭ dudek? Kiu manĝis oranĝojn en la lernejo (shule)? Ĉu vi aŭdas tion? Ĉu vi helpis la knabinojn? Kiu rompis la seĝon? Kion vi trinkas? Kie estas la libro, kiun (ambacho) vi aĉetis?

Somo la saba

56. Alama ya mtendewa -*N*

USIITUMIE alama *-n* ya mtendewa:

1. mwishoni mwa mtendaji:
Mi manĝas (siyo: *Min manĝas*).
2. katika sentensi zenye *est-* kama kitenzi:
ĝi estas teo (siyo: *teon*),
3. mwishoni mwa maneno yanayofuata viunganishi vihusishi kama *al* na vinginevyo:
unaweza kusema (au kuandika)
Mi dankas vin
au *Mi dankas al vi*,
lakini **huruhusiwi** kusema (au kuandika) *Mi dankas al vin*.
unaweza kusema (au kuandika) *Li vokas nin*.
au *Li vokas al ni*.
huruhusiwi kusema (au kuandika) *Li vokas al nin*.

57. Upatanishaji wa kisarufi

Vivumishi vingi vya Kiswahili vinabadilika kufuata mianzo ya majina katika ngeli zake. Vivumishi vya Kiesperanto huchukua

viambishi **-j**, **-n**, **-jn** kulingana na majina vinayoyasifu:

Hiki ni kitabu kipyá	<i>Tiu ĉi estas nova libro</i>
Hivi ni vitabu vipya	<i>Tiuĵ ĉi estas novaj libroj</i>
Nimekinunua kitabu kipyá	<i>Mi aĉetis novan libron</i>
Nimevinunua vitabu vipya	<i>Mi aĉetis novajn librojn</i>

58. Zoezi

Tafsiri:

Li prenis (-chukua) du ruĝajn librojn, kaj tenis (-shika) ilin en la mano. Li skribis al mi longan leteron kaj bildan poŝtkarton (kadi ya kupelekea kwa njia ya posta). Ni aŭdis tri belajn kantojn. Ili donis al mi blankan paperon. Ĉu li havas brunajn harojn (nywele) aŭ nigrajn? Vi ne viŝis la nigran tabulon (ubao). Mi legis tre interesajn (-a kuvutisha) librojn.

59. KIA na KIU

Viulizi **kia** na **kiu** huchukua viambishi **-j**, **-n**, **-jn** kulingana na majina vinayoyahusu:

Kian infanon vi amas?

vi ni kiima,

Kian infanon ni yambwa

Bonan. Mi amas bonan infanon. Kiajn infanojn vi amas?

Bonajn.

60. Kiambishi tamati -OS

Kiambishi hiki cha njeo kinaonyesha wakati ujao wa kitenzi, sawasawa na **-ta-** au **-taka-** kwa Kiswahili:

Mi estos

Nitakuwa

Li estos

Atakuwa

Mi skribos baldaŭ.

Tutaandika hivi karibuni.

<i>Ŝi venos, ĉu ne?</i>	Atakuja , sivyo?
<i>Ĉu vi ludos kun mi?</i>	(Je,) Utacheza pamoja nami?

61. Vielezi vya wakati

Vielezi vinavyoeleza kitendo **wakati** kinapotendeka:

<i>Hieraŭ li kantis.</i>	Jana aliimba.
<i>Hodiaŭ li kantas.</i>	Leo anaimba.
<i>Morgaŭ li kantos.</i>	Kesho ataimba.

62. *KIAM?* = lini? wakati gani?

Ukitaka kuuliza tendo fulani linatendeka au limetendeka au litatendeka lini, kwa Kiswahili unaweza kutumia **lini?** au **wakati gani?**.

Kiesperanto kinatumia *KIAM?*

Mfano:

<i>Kiam ŝi venis?</i>	Alikuja lini?
<i>Ŝi venis hieraŭ</i>	Alikuja jana .

63. Zoezi

Tafsiri:

Kiam ŝi iros (-enda)? Ŝi iros morgaŭ. Hodiaŭ estas mardo (jumanne), hieraŭ estis lundo (jumatatu), kaj morgaŭ estos merkredo (jumatano). Hieraŭ estis jaŭdo (alhamisi), morgaŭ estos sabato kaj hodiaŭ estas vendredo. Dimanĉo (jumapili) estas ripoza tago.

64. Umilikishi

Ukitaka kuonyesha kuwa kiumbe au kitu fulani kinamilikiwa, lazima utumie vivumishi vya sifa za umilikishi. Vipashio hivyo vinavyoitwa viwakilishi vimilikishi vinatangulia jina la kiumbe au kitu kimilikiwacho na vinawakilisha kiumbe au kitu kimilikicho. Kwa sababu vimilikishi vinaonyesha mmiliki, vina-patikana na viwakilishi vya mtendaji vyenye kiambishi cha vivumishi **-a**:

<i>mi</i>	mimi	<i>mi</i>	-angu
<i>vi</i>	wewe	<i>via</i>	-ako
<i>li</i>	yeye	<i>lia</i>	-ake
<i>ŝi</i>	yeye	<i>ŝia</i>	-ake
<i>ĝi</i>	yeye	<i>ĝia</i>	-ake
<i>ni</i>	sisi	<i>nia</i>	-etu
<i>vi</i>	ninyi	<i>via</i>	-enu
<i>ili</i>	wao	<i>ilia</i>	-ao
<i>ili</i>	wao	<i>ilia</i>	-ake ³

65. Vimilikishi

Viwakilishi vimilikishi hufuata kanuni zote za vivumishi. Changuza matumizi ya vimilikishi katika mifano yafuatayo:

<i>mia mapo</i>	ramani yangu
<i>miaj mapoj</i>	ramani zangu
<i>via amiko</i>	rafiki yako / yenu
<i>viaj amikoj</i>	rafiki zako / zenu
<i>lia domo</i>	nyumba yake
<i>liaj domoj</i>	nyumba zake

³kuhusu: vitu au miti

<i>ilia filo</i>			mtoto wao
<i>iliaj filoj</i>			watoto wao
<i>ĝia floro</i>			ua lake
<i>ĝiaj floroj</i>			maua yake
<i>ŝia frato</i>			ndugu / kaka yake
<i>ŝiaj fratoj</i>			ndugu / kaka zake
<i>mia bovo</i>			ng'ombe wangu
<i>miaj bovoj</i>			ng'ombe wangu
<i>via fadeno</i>			uzi wako / wenu
<i>viaj fadenoj</i>			nyuzi zako / zenu
<i>mia loko</i>			mahali pangu / kwangu / mwangu
<i>miaj lokoj</i>			mahali pangu / kwangu / mwangu
<i>ĝia arbo</i>	mti wake	<i>ĝiaj arboj</i>	miti yake
<i>via kapo</i>	kichwa chenu	<i>viaj kapoj</i>	vichwa vyenu
<i>ilia vojo</i>	njia yake	<i>iliaj vojoj</i>	njia zake

*Li uzas mian inkon.
Johano aĉetis nian katon.
Kiu havas miajn librojn?
Viaj libroj estas tie.*

Anatumia vino wangu.
John alinunua paka wetu.
Nani ana vitabu vyangu?
Vitabu vyako vipo pale.

Mifano mingine:

<i>Mi posedas libron.</i>	Ninamiliki kitabu.
<i>La libro estas mia.</i>	Kitabu ni changu.

Tiu estas mia libro. Hiki ni kitabu changu.

Vi posedas seĝon. La seĝo estas via. Tiu estas via seĝo. Unamiliki kiti. Kiti ni chako. Hiki ni kiti chako.

Li posedas tablon. La tablo estas lia. Tiu estas lia tablo. (mwanamume) Anamiliki meza. Meza ni yake. Hii ni meza yake.

Ŝi posedas florojn. La floroj estas ŝia. Tiuj estas ŝiaj floroj. (mwanamke) Anamiliki maua. Maua ni yake. Haya ni maua yake.

Ni posedas domon. La domo estas nia. Tiu estas nia domo. Tunamiliki nyumba. Nyumba ni yetu. Hii ni nyumba yetu.

(ninyi) *Vi posedas bildojn. La bildoj estas viaj. Tiuj estas viaj bildoj.* Mnamiliki picha. Picha ni zenu. Hizi ni picha zenu.

Ili posedas katojn. La katoj estas iliaj. Tiuj estas iliaj katoj. Wanamiliki paka. Paka ni wao. Hawa ni paka wao.

Hata vitu vinaweza kumiliki vitu vingine:

La domo posedas tri fenestrojn. Tiuj estas ĝiaj fenestroj. Nyumba ina madirisha matatu. Madirisha matatu ni yake. Haya ni madirisha matatu yake.

La libro posedas bildojn. Tiuj estas ĝiaj bildoj. Kitabu kina picha. Picha ni zake. Hizi ni picha zake.

La arboj havas foliojn. Tiuj estas iliaj folioj. Miti ina majani. Majani ni yake. Haya ni majani yake.

Kumbuka matumizi ya kiambishi cha mtendewa. Hakitu-

miwi kwenye kitenzi *est-*.

66. **KIAL?** = Kwa nini? ... **ĈAR** = Kwa sababu, kwa kuwa

Ukitaka kuuliza sababu za tendo fulani, kwa Kiswahili unaweza kutumia **kwa nini?** au **kwa sababu gani?** au **kwa kuwa?**.

Kwa Kiesperanto tunatumia **KIAL?** na tunajibu kwa kutumia **ĈAR**.

Tafsiri:

Kial vi venis? *Mi venis, ĉar vi vokis. Kial vi silentas?* (-nyamaa) *Mi silentas, ĉar mia filino dormas. Kial ŝi kantas?* *Ĉar ŝi estas feliĉa. Kial vi ridas? Ĉar ankaŭ (pia) mi estas feliĉa. Kial vi ne lernis la lecionon?* (somo) *Kial la instruisto punis la knabojn? Kial vi tuŝis lin? Kial vi manĝas verdajn bananojn?*

67. Zoezi

Tafsiri:

Viaj taskoj estas simplaj. Ĉu vi vidis mian onklinon? Kial vi ne kombas (-chana) viajn harojn? Kie estas miaj paperoj? Kiu manĝis miajn fiŝojn? Mi lernos miajn lecionojn. Ni vidos nian reĝinon. Kiam vi skribas viajn leterojn?

Somo la nane



68. Kikati cha udogo *-ET-*

Kwa kutumika kiambishi hicho cha ndani inawezekana kuonyesha udogo. Inawezekana kuonyesha udogo wa vivumishi, vitenzi, majina, na vielezi kwa kutumia kikati *-et-* (waswahili kadhaa wanatumia kiambishi awali **ka-**):

<i>lampo</i>	taa	<i>lampeto</i>	kijitaa
<i>libro</i>	kitabu	<i>libreto</i>	kijitabu
<i>fingro</i>	kidole	<i>fingreto</i>	kijidole
<i>ŝuo</i>	kiatu	<i>ŝueto</i>	kijiatu
<i>monto</i>	mlima	<i>monteto</i>	kilima
<i>ridi</i>	kucheka	<i>rideti</i>	kutabasamu
<i>bela</i>	-zuri	<i>beleta</i>	-zuri kidogo

69. Kikati cha ukubwa *-EG-*

Kinyume cha fungu iliopita hapa utajifunza kuonyesha ukubwa. Kufanya hivyo, lazima utumie kikati cha ukubwa *-eg-*:

<i>domo</i>	nyumba	<i>dometo</i>	kijumba
		<i>domego</i>	jumba
<i>urbo</i>	mji	<i>urbeto</i>	kijiji
		<i>urbego</i>	jiji

<i>pordo</i>	mlango	<i>pordeto</i>	kijilango
		<i>pordego</i>	jilango, lango
<i>tablo</i>	meza	<i>tableto</i>	kijimeza
		<i>tablego</i>	jimeza
<i>manĝi</i>	kula	<i>manĝeti</i>	kula kidogo kidogo, kumega
		<i>manĝegi</i>	kula mno sana, kujivimbisha
<i>plori</i>	kulia	<i>ploreti</i>	kulialia
		<i>ploreĝi</i>	kulia kwa kelele (kwikwi)
<i>trinki</i>	kunywa	<i>trinketi</i>	kunywa kidogo kidogo
		<i>trinkeĝi</i>	kunywa kwa pupa
<i>malsana</i>	-gonjwa	<i>malsaneta</i>	-gonjwa kidogo
		<i>malsanega</i>	-gonjwa sana (mahtuti)

70. Zoezi

Tafsiri:

La akvo estas nur varmeta, sed mi deziras (-taka) akvon varmegan. Mia karega patrineto venos morgaŭ. Lia hundo estas grandega. La knabeto estis bonega hieraŭ. Vi havas malpuregajn manojn. Ilia fileto ripozas en liteto. Mi amegas mian patron. Hodiaŭ ŝi dormetas post (baada ya) la manĝego. Mi estas lacega (-chovu sana).

71. Kihusishi *DE*

Neno *de* linafanya kazi mbalimbali: huongeza kitenzi, jina, n.k. Mara nyingi linatafsiri: **wa, ya, la, cha, vya, za**. Chun-guza matumizi yake katika sentensi zifuatazo:

Ĉapelo pendas de hoko.

Kofia imetundikwa
changoni.

<i>Rivero fluas de montoj al maro.</i>	Mto huenda kuanzia mlimani kuelekea baharini.
<i>Birdo saltis de unu branço al la alia.</i>	Ndege aliruka toka tawi moja mpaka tawi jingine.
<i>La libro de Petro estas sur la tablo.</i>	Kitabu cha Peter kipo mezani.

72. **DIRU AL MI**, = Uniambie.

Sasa tafsiri:

Diru al mi, kiu vi estas?

Diru al mi, kie vi loĝas (-kalia)?

Diru al mi, kion vi faras (-fanya)?

Diru al mi, kiun vi amas?

Diru al mi, ĉu vi havas fratojn kaj fratinojn?

Diru al mi, kiom da fratoj vi havas?

Diru al mi, kiom da fratinoj vi havas?

Diru al mi, ĉu vi havas edzinon (mke)?

Diru al mi, kiom da filoj kaj filinoj vi havas ?

73. Vionyeshi

Ukisema *ninampenda msichana huyu* hilo neno *huyu* laitwa kionyeshi, kwa sababu latoa ishara juu ya yule tunayemzungumza habari zake: yaani latuelekeza ama kutuonyesha huyo msichana.

Jifunze kwa njia ya sentensi zifuatazo vionyeshi vichache vya Kiesperanto. Kumbuka kwamba kila kiashirio cha Kiesperanto kina kianzio cha **t-** (je, unakumbuka kwamba viulizi vinaanza kwa **k-**?):

Kio?

Nini?

Tio

Kile. Ile.

Kio estas tio? Kile ni nini?
Kile ni kitu
gani?

Kiu? Nani? -pi? **Tiu** Yule. Ile
Kiun bananon Unataka ndizi
vi preferas? ipi?

Mi amas tiun. Ninampenda yule.
Mi malamas tiun viron. Ninamchukia mtu yule.
Kiun libron vi legas? Unasoma kitabu kipi? /
gani?
Mi uzos tiun plumon. Nitatumia kalamu ile.

74. Neno **ĈI**

Vionyeshi ulivyojifunza katika kifungu cha hapa juu hutumika kuonyesha mtu (au kitu, n. k.) ambaye yuko mbali na msemajji. Vionyeshi vile vile pamoja na neno **ĉi** hutumika kuonyesha kiumbe (mtu, kitu, n.k.) ambacho kiko karibu na msemajji:

huyu	ĉi tiu	yule, huyo	<i>tiu</i>
hiki	ĉi tio	kile, hicho	<i>tio</i>
hapa	ĉi tie	pale, hapo	<i>tie</i>

na kadhalika.

75. Zoezi

Tafsiri:

Li ne estas tie, li estas ĉi tie. Tio estas fenestro; ĉi tio estas tablo. Mi ne legis tiun libron, sed mi legis ĉi tiun. Tiuj viroj. Ĉi tiuj viroj. Mi legis tiujn librojn. Mi legas ĉi tiujn librojn. Diru al mi, kiu estas tiu bela knabeto? La libretoj

estas sur ĉi tiu tablo. Ĉu vi vidas tiujn homojn. Kio estas ĉi tio ? Tiuj infanoj lernas aritmetikon (mahesabu), ĉi tiuj lernas geografion (jiografia). Kiu estis en la ĉambro? Kiu estis en la ĉambro? Kiujn librojn vi prenis.

76. Virejeshi

Kwa Kiswahili hutumika viambishi virejeshi vya namna mbili:

a. namna ya kwanza ni kikati: **-vyo-**, **-ye-**, n.k. kwa mfano:

Myuzi zilizokatika ...

Msichana aliyekuja ...

b. namna ya pili ni neno **amba-** kwa viambishi **-ye**, **-vyo**, n.k. kwa mfano:

Mahali **ambapo** ni pazuri ...

Kwa Kiesperanto hutumika maneno yale yale unayoyajua kama viulizi: **kiu**, **kia**, **kio**, **kie**, ...

Tazama yanavyotumika:

Msichana alikuja jana. *Knabino venis hieraŭ.*

Msichana amekufa. *Knabino mortis.*

Msichana yupi? *Kiu knabino?*

Msichana aliyekuja jana. *La knabino **kiu** venis hieraŭ.*

Msichana aliyekuja jana amekufa.

*La knabino, **kiu** venis hieraŭ, mortis.*

Nilinunua kitabu jana. *Mi aĉetis libron hieraŭ.*

Nimeleta kitabu. *Mi portis libron.*

Umeleta kitabu kipi? *Kiun libron vi portis?*

Nimeleta kitabu nilicho-*Mi portis la libron, **kiun** nunua jana. *mi aĉetis hieraŭ.**

Sasa tazama sentensi zingine:

Nitamwambia atakapokuja.	<i>Mi parolos al li kiam li venos.</i>
Najua anavyofanya.	<i>Mi scias kiel li faras.</i>
Fanya upendavyo.	<i>Faru kiel vi deziras.</i>
Atakapokuja tutaenda sokoni.	<i>Kiam li venos, ni iros al bazaro.</i>

77. Zoezi.

Tafsiri:

Kie estas la hundo, kiun vi aĉetis hieraŭ? Ĝi dormas. Kion vi faras, kiam vi estas feliĉa? Kiam mi estas feliĉa, mi kantas. Kial vi ne estis ĉi tie, kiam ili venis? Ĉar mi estis en Daresalamo, kiam ili venis. La knabeto timegis (-ogopa sana), kiam li vidis la bestegon.

Somo la tisa

78. Kikati -IST-

Kiambishi hicho cha ndani hutumika kuonyesha afanyaye kazi fulani kwa mshahara. Tazama mifano hii:

mchungaji	<i>paștisto,</i> <i>paștistino</i>	kuchunga	<i>paști</i>
mwimbaji	<i>kantisto,</i> <i>kantistino</i>	kuimba	<i>kanti</i>
mchoraji	<i>pentristo,</i> <i>pentristino</i>	kuchora	<i>pentri</i>
mpagazi	<i>portisto,</i> <i>portistino</i>	kupagaa	<i>porti</i>
mlezi	<i>vartisto,</i> <i>vartistino</i>	kulea	<i>varti</i>
mwizi	<i>ștelisto,</i> <i>ștelistino</i>	kuiba	<i>șteli</i>
mfanya kazi	<i>laboristo,</i> la- <i>boristino</i>	kufanya kazi	<i>labori</i>
kiongozi	<i>gvidisto,</i> <i>gvidistino</i>	kuongoza	<i>gvidi</i>
hakimu, jaji	<i>juđisto,</i> <i>juđistino</i>	kuhukumu	<i>juđi</i>

79. Zoezi

Andika majina ya wafanyakazi wa kiume na wa kike yana-
yoweza kutokana na maneno haya yafuatayo: *boto* (buti), *dento*
(jino), *baki* (kuoka).

Tafsiri:

ĉapelisto, *floristo*, *ĝardenisto*, *vendisto*, *lignisto* (*ligno* =kipande
cha mti, ukuni).

Rudia maneno ya hapa juu ukitumia kikati **-in-**, halafu
tafsiri maneno haya mapya.

80. Kikati **-IL-**

Kikati hiki huonyesha chombo ambacho hufanywa kazi kwa
njia yake: zana, ala:

kifunguo	<i>ŝlosilo</i>	kufungua	<i>malŝlosi</i>
mtego	<i>enkaptilo</i>	kutega	<i>enkapti</i>
ponyo	<i>kuracilo</i>	kuponya	<i>kuraci</i>
shoka	<i>hakilo</i>	kutema	<i>haki</i>
sindano ya	<i>kudrilo</i>	kushona	<i>kudri</i>
kushonea			
rula	<i>liniilo</i>	mstari	<i>linio</i>
mchezo (kititia)	<i>ludilo</i>	kucheza	<i>ludi</i>
kisu	<i>tranĉilo</i>	kukata	<i>tranĉi</i>

81. **PER** = kwa, kwa njia ya.

Aliua nyoka kwa bunduki = *Li mortigis serpenton per pafilo*.

82. Zoezi

Tafsiri:

Ni hakas per hakilo. Kial vi kombas viajn harojn per forko,

kaj ne per kombilo? Tio estas la viŝilo, per kiu mi viŝas la tabulon.

83. Zoezi

Ukitumia maneno haya hapa chini pamoja na kikati cha zana **-il-** tafsiri sentensi zifuatazo maneno yenyewe: *tondi* (kunyoa), *fosi* (kuchimba), *presi* (kuchapa), *segi* (kupasulia);

Wote hunyoa kwa mkasi. Wote huchimba kwa sepetu. Wote huchapisha kwa mtambo wa kupigia chapa. Wote hupasulia kwa msumeno.

Fuata mfano huu:

Wote hunyoa kwa mkasi = *Ĉiuj tondas per tondilo.*

84. Kikati **-AR-**

Kikati hiki huonyesha jumuiko au mkusanyiko wa viumbe vyenye aina moja tu:

<i>arbo</i>	mti	<i>arbaro</i>	msitu, mwitu
<i>kampo</i>	shamba	<i>kamparo</i>	shamba
<i>libro</i>	kitabu	<i>libraro</i>	maktaba, jumuiko la vitabu
<i>mapo</i>	ramani	<i>maparo</i>	atlas
<i>ŝtupo</i>	kipago, kidaraja	<i>ŝtuparo</i>	ngazi
<i>vagono</i>	behewa	<i>vagonaro</i>	gari la moshi
<i>vorto</i>	nen	<i>vortaro</i>	kamusi

85. Zoezi

Tafsiri ukitumia kikati **-ar-**:

jamii ya rafiki, kundi la ng'ombe, jamii ya vyumba, kundi la ndugu, diwani la nyimbo, kundi la vijana, kundi la kondoo,

jamii ya meli.

86. Vielezi vya wakati

Mpaka sasa umeshajifunza maneno: *baldaŭ*, *nun*, *hierauŭ*, *hodiaŭ*, *morgaŭ*. Maneno haya huonyesha kitendo wakati kilipotendeka. Tunaita maneno haya “vielezi vya wakati”.

Jifunze mengine:

ĉiam = daima, milele, bila ya kukoma

neniam = abadani, kamwe, hata mara moja

jam = zamani.

ANGALIA kwamba:

1) kielezi *neniam* hakitumiki kama kitenzi cha Kiesperanto ni katika hali ya kutotenda, yaani kama kitenzi kinatanguliwa kwa neno *ne*.

Mfano:

Mi ne kuiras

Sipiki (sasa hivi)

Mi neniam kuiras

Sipiki hata mara moja.

(kwa kawaida)

2) wazo la “hata kidogo” linatolewa kutoka katika Kiesperanto kwa neno *neni-o-m siyo* kwa neno *neni-a-m*.

Chunguza matumizi ya vielezi vya wakati katika sentensi zifuatazo:

Li jam venis.

Amekwisha fika.

Ameshafika.

Mi jam pagis

Nimelipa zamani.

Ameshalipa zamani.

*Tiu homo neniam
kontentiĝas.*

Mtu huyu haridhiki

abadani.

Mi neniam venos.

Sitakuja abadani.

87. Zoezi

Tafsiri:

Ĉu vi baldaŭ venos? Jes, mi venos hodiaŭ. Ĉu la teo estas preta nun? Mi jam skribis du leterojn. Kiu venos morgaŭ? Kial la ĝardenisto ne venis hieraŭ? Hodiaŭ mi aĉetos segilon. Mi jam havas tranĉilon. Mi neniam uzis hakilon. Ne nun, sed baldaŭ. Mi ĉiam kantas kiam mi estas feliĉa.

88. Vielezi vingine

Kwa jumla vielezi ni maneno yanayoeleza vile vitendo vilivyotendeka, yaani yaeleza kitendo jinsi kilivyotendeka, mahali kilipotendeka, wakati kilipotendeka, n.k.

Tukisema: “amekuja **polepole**”, “unasoma **vizuri**”, “ameingia **hapa**”, “njoo **kesho**”, n.k. huwa tumetumia vielezi; yaani:

- kielezi cha mahali (huonyesha kitendo mahali kilipotendeka): **hapa**.
- kielezi cha wakati (huonyesha kitendo wakati kilipotendeka): **kesho**.
- vielezi vya namna (huonyesha kitendo jinsi kilivyotendeka): **polepole**, **vizuri**.

Hapa chini vipo vielezi kadhaa vya namna:

<i>bele</i>	vizuri	<i>lerte</i>	kwa ustadi
<i>bone</i>	vyema	<i>malbone</i>	vibaya, kwa kosa
<i>hele</i>	kwa uangavu	<i>simple</i>	tu, peke yake, rahisi

89. Kiambishi tamati -E

Uliposoma vielezi vilivyopita uligundua kwamba maneno haya yote (yaani ya kifungu cha 88) huwa yametumia kiambishi kile kile: *-e*. Basi, kwa Kiesperanto kila neno likitumia kiambishi tamati *-e* linaweza kufanya kazi ya kielezi. Pia kila kielezi cha namna lazima kiwe na kiambishi hicho cha *-e*. Kwa mfano:

<i>rapid-</i>	<i>rapida</i>	-epesi, -a upesi	<i>rapide</i>	upesi
<i>saĝ-</i>	<i>saĝa</i>	-a busara	<i>saĝe</i>	kwa busara

Vielezi vyenye kiambishi *-e* ulivyovisoma mpaka sasa ni: *eble, kompreneble, efektive*.

90. Zoezi

Tafsiri vielezi vifuatavyo:

kwa utamu, kwa wazi (au: kwa dhahiri), kwa kelele (au: kwa sauti kubwa), kwa polepole (au: kinyerenyere), kwa kweli (au: kwa moyo, kiaminifu),

kwa kutumia maneno ya orodha ya hapa chini:

dolĉa -tamu

klara wazi, dhahiri

laŭta -a kelele, -enye sauti kubwa

malrapida polepole

sincera -aminifu

Somo la kumi

91. Vielezi vingine vya mahali

Hapa chini vipo vielezi vingine vya mahali:

êie = kila mahali, popote

nenie = popote (katika ukanushaji tu)

for = mbali *fora* = -a mbali (kivumishi)

Chunguza matumizi ya vielezi hivi vya mahali katika sentensi zifuatazo:

Mi serêos êie.

Nitatafuta kila mahali.

La homo vivas êie.

Yule mtu anaishi popote.

Mi trovis bananon nenie.

Sikukuta ndizi popote.

Mi venis el fora loko.

Nimetoka mahali pa mbali.

92. Zoezi

Tafsiri:

Li êiam parolas bone. Mia kuzino neniam skribas klare. Tiu virino êiam kantas gaje (gaj- = -enye ukunjufu). Li parolas tre saêe. Mi serêis lin êie, sed trovis lin nenie. Ili vivas tre simple. La êtelisto rapide kuris for. Mi ofte (mara nyingi) vidis la êipojn. Li malofte uzas vortaron. Kompreneble, mi ne iros.

93. Uundaji wa maneno

Sasa umeshaelewa kabisa uundaji wa maneno tulioeleza pia katika kifungu cha 5; bila shaka unafahamu kwamba kutoka mzizi **VIV-** unaweza kuunda maneno mengi, kwa mfano:

maisha	<i>VIVo</i>	(jina)
-enye uhai, -hai, -enye	<i>VIVa</i>	(kivumishi)
kuishi		
kwa uhai, kwa maisha	<i>VIVe</i>	(kielezi)
kuishi	<i>VIVi</i>	(kitenzi)
niliishi, nimeishi	<i>mi VIVis</i>	(wakati uliopita)
ataishi	<i>li VIVos</i>	(wakati ujao)
atakayeishi	<i>li, kiu VIVos</i>	(wakati ujao)
n.k.		

94. Zoezi

Je, maneno mangapi unaweza kuunda kutoka mizizi ya hapa chini?

am-, esper-, telefon-

Kwa mfano:

ami=kupenda, *esperi* =kutumaini, *telefono* =simu, sasa endelea wewe mwenyewe ukiandika maneno unayoyaunda pamoja na tafsiri zao.

95. Kiambishi tamati -U

Umeshajifunza msembo *Diru al mi*, “uniambie” (taz. kifungu cha 72). Basi, ukumbuke kwamba amri au matakwa au maombi unaweza kutoa ukitumia kiambishi cha **-u** kwenye mzizi:

<i>legu!</i>	soma!	<i>penu!</i>	jitahidi!
	someni!		jaribu!

silentu! nyamaza! *skribu!* andika!

lakini kwa upole na ukarimu itafaa kutumia msembo

bonvolu. . . -i,

kwa mfano:

Venu al mi!

Njoo kwangu!

Bonvolu veni al mi!

Tafadhali njoo kwangu!

96. Zoezi

Rudia sentensi zifuatazo ukitumia neno *bonvolu*:

Finu vian taskon! (Maliza kazi yako!), *Atentu kaj aŭskultu!*
(Angalia usikilize!), *Ne rigardu al ŝi!* (Usimtazame!), *Ne parolu dum la leciono!* (Usizungumze wakati wa kipindi!).

97. Vitenzi maalumu

ANGALIA sana. Ujifunze misemo ifuatayo yenye vitenzi *povi*,
devi, *voli*, *deziri*:

Mi povas iri.

Ninaweza kwenda.

Mi devas iri.

Inanipasa kwenda.

Au: Inanibidi kwenda.

Au: Yanilazimu kwenda.

Au: Sina budi kwenda.

Au: Ninalazimika kwenda.

Au: Lazima niende.

Au: Ni lazima niende.

Au: Ninatakiwa niende.

Mi volas iri.

Nataka kwenda.

Mi deziras iri.

Napenda kwenda.

Mi ne povas iri.

Siwezi kwenda. (LAKINI:

Siwezi = *Mi ne bonfartas.*)

Ĉu vi povos iri?

Je, utaweza kwenda?

Li ne povis iri, ĉu?

Hakuweza kwenda, sivyo?

98. Neno **JEN**

UKIULIZA *Kie la libro estas?* au *Kie estas la libro?* (Kile kitabu kipo wapi?) unaweza kujibiwa *Jen ĝi estas!* (Ndicho hiki! Ndicho kitabu!). Kwa kawaida inawezeka kuacha neno *estas*, yaani unaweza kujibu ***Jen ĝi!*** tu.

99. Misemo

Ujifunze misemo ifuatayo:

Kuna hali gani nje?	<i>Kia estas la vetero ekstere?</i>
Kumefunga mawingu.	<i>Nubiĝis.</i>
Kumekuwa kweupe.	<i>Klariĝis.</i>
Inanyesha mvua.	<i>Pluvas.</i>
Kunanyesha mvua.	
Inaanguka theluji.	<i>Neĝas.</i>
Kunakucha.	<i>Tagiĝas.</i>
Kumekucha.	<i>Tagiĝis.</i>
Kumepambazuka.	
Inaingia giza.	<i>Noktiĝas.</i>
Tulingoja hata imeingia giza.	<i>Ni atendis ĝis noktiĝo.</i>

Basi, kwenye misemo kuhusu hali ya hewa kwa Kiesperanto haitumiki kiwakilishi chochote cha mtendaji. Pia katika msemu ufuatao:

Ŝajnas al mi, ke ...

Naona kwamba...

100. Majina ya heshima

Kama Hamisi Saleh amemwoa Fatuma Kapinga na wao wamezaa Manase bin Hamisi Saleh, basi kwa Kiesperanto:

Bibi Saleh	ni <i>Sinjorino</i> (<i>S-ino</i> ni kifupisho chake) <i>Kapinga</i> .
Mama Manase	ni <i>Sinjorino Kapinga</i> au <i>Sinjorino Fatuma</i> .
Bwana Hamisi	ni <i>Sinjoro (S-ro) Saleh</i> au <i>Sinjoro Hamisi</i> .
Bwana Manase	ni <i>Sinjoro Saleh</i> au <i>Sinjoro Manase</i> .
Bibi Nyanjala binti Hamisi Saleh	ni <i>Sinjorino (S-ino) Saleh</i> , au <i>Fraŭlino (f-ino) Saleh</i> , au <i>Sinjorino Njanĝala</i> , au <i>Fraŭlino Njanĝala</i> .

101. Maamkio

ANGALIA matumizi haya ya maneno *Sinjoro*, *Sinjorino*, *Fraŭlino*:

<i>Saluton, Sinjoro!</i>	Jambo, bwana! Jambo, kaka!
<i>Saluton, Sinjorino!</i>	Jambo, mama! Jambo, bibi!
<i>Saluton, Fraŭlino!</i>	Jambo, bibi! Jambo, dada!

Lakini afadhali utumie neno *saluton* ukisalimu rafiki tu, kama sivyo afadhali utumie maneno yafuatayo:

Kuanzia asubuhi mpaka adhuhuri:

Bonan matenon! Sabalkheri! Habari za asubuhi?

Wakati wa mchana baada ya adhuhuri:

Bonan tagon! Sabalkheri! Habari za mchana? Habari

za leo?

Jua likianza kuchwa:

Bonan vesperon! Msalkheri! Habari za jioni? Habari za usiku?

Jua likiisha kuchwa aghalabu katika kuachana:

Bonan nokton! Lala unono! Usiku mwema! Msalkheri!

Maneno haya hutumika pia ukiachana. Katika kuachana na rafiki hutumika pia *Ĝis revido!* (Tutaonana! Kwa heri! Kwa herini!)

102. Misemo mingine

Parolu al la sinjoro.

Ongea na bwana yule.

Mi konas tiun sinjorinon.

Namjua msichana (dada, binti) yule.

Ŝi estas ĉarma fraŭlino.

Yeye ni msichana (dada) mpendezi.

103. Vivumishi vingine

Kelkaj fraŭlinoj kantos.

Baadhi ya wasichana wataimba.

Multaj floroj estas ruĝaj, aliaj estas bluaj.

Maua mengi ni mekundu, mengine ni buluu.

104. Zoezi

Tafsiri ukitumia kamusi:

Mombaso, la 17-an de Decembro 1917-a

Kara amikino,

mi povas legi vian leteron; ĝi estas en la internacia lingvo

(lugha ya kimataifa) *Esperanto. Ankaŭ mi havas lernolibreton. Per la helpo de tiu libreto mi jam lernis sufiĉe por skribi ĉi tiun leteron. La libro estas tre klara, kaj mi lernas rapide. Esperanto estas tre simpla kaj interesa. Ankaŭ via frato devas aĉeti libron kaj lerni la lingvon.*

Hieraŭ mi ricevis belan ilustritan (-enye picha) poŝt-karton de knabo, kiu loĝas en Nederlando (Uholanzi), kaj mi povis legi ĝin facile per la helpo de vortareto. Morgaŭ mi skribos leteron al japana knabo (mvulana mjapani). Mia fratino ofte korespondas kun knabinoj en aliaj landoj. Ŝi nun havas multajn poŝtkartojn kaj fremdajn poŝtmarkojn (stempu).

*Kun koraj salutoj (Kwa salamu za moyoni),
Tumaini Mafuru*

105. Zoezi:

Tafsiri ukutumia kamusi:

Londono, la 25-an de Julio 1982-a

Mia kara onklino,

*mi dankas vin pro (kwa)la bela pupo, kiun vi sendis al mi. Mi multe amas ĝin: ĝi havas blujajn okulojn kaj ruĝajn van-
gojn, kaj ĝi povas fermi la okulojn.*

Mi estas tre feliĉa ĉi tie. La floroj en la ĝardeno estas belaj. Kelkaj pom-arboj (mtufaha wa kizungu) estas en la ĝardeno, sed la frukto ne estas matura. Estas (Wapo)kokoj kaj kokinoj sur la korto, kaj ŝafoj kaj bovinoj sur la granda kampo. Ni ludas en la ĝardeno. Kiam (taz. vifungu vya 76 na vya 87: Wakati -po-, Ambapo)mi estas laca, mi sidas sur benko sub la arboj kaj legas. La birdoj kantas sur la arboj, kaj belaj papilioj flugas en la ĝardeno. Mia avo ofte sidas sur granda seĝo apud la fenestro, kaj legas gazeton aŭ libron. Li havas multajn librojn. Sed mi devas fini mian leteron, ĉar mia kara avino diras, ke (kwamba)mi devas nun iri al la lito. Bonan nokton!

Via amanta (akupendaye)nevino,

Ethel Brown

Viambishi vyote

Viambishi awali

bo	<i>ujamaa kutokana na ndoa</i>		
Mf. bopatroj	<i>mama na baba mkwe</i>		
dis	<i>utatawanyiko, kusambaza</i>		
Mf. disdono	<i>usambasaji</i>	disigi	<i>kutenga</i>
ek	<i>mwanzo wa hatua, ghafla</i>		
Mf. ekflori	<i>kuchanua ghafla</i>		
eks	<i>kukomesha kazi</i>		
Mf. eksministro	<i>waziri wa zamani</i>		
fi	<i>dharahu</i>		
Mf. fiwortoj	<i>matusi</i>		
for	<i>umbali</i>		
Mf. forpreni	<i>kuondoa</i>		
ge	<i>inahusu jinsia zote</i>		
Mf. gepatroj	<i>baba na mama</i>		
mal	<i>Taz. uk. 19</i>		
mis	<i>kosa</i>		
Mf. miskompreno	<i>kutoelewa</i>		
pra	<i>umbali kwa wakati</i>		
Mf. praavo	<i>mhenga</i>		
re	<i>kurudia tena</i>		
Mf. rediru	<i>sema tena</i>		

Vikati

aĉ	<i>kitu au mtu mbaya, -a kuchukia</i>
-----------	---------------------------------------

Mf.	<i>homaĉo</i>	<i>mtu mbaya</i>
ad	kitendo kinachoendelea	
Mf.	<i>dirado</i>	<i>kusemasema</i>
aĵ	kitu	
Mf.	<i>belajo</i>	<i>kitu kizuri</i>
an	mwana-	
Mf.	<i>partiano</i>	<i>mwanachama</i>
ar	Taz. uk. 59	
eb1	uwezekano (-ika)	
Mf.	<i>manĝebla</i>	<i>inayolika</i>
ec	ubora wa kufikirika (u-)	
Mf.	<i>beleco</i>	<i>uzuri</i>
eg	Taz. uk. 51	
ej	mahali	
Mf.	<i>manĝejo</i>	<i>mahali pa kula</i>
em	<i>tabia, mwelekeo, hamu</i>	
Mf.	<i>parolema</i>	-a maneno mengi
end	kinachotakiwa kifanywe	
Mf.	<i>skribenda</i>	-a lazima kuandika
er	kipande kidogo, chembe	
Mf.	<i>fajrero</i>	<i>cheche</i>
estr	mkuu	
Mf.	<i>vilagestro</i>	<i>mwenyekiti wa kijiji</i>
et	Taz. uk. 51	
id	mtoto wa mtu au mnyama	
Mf.	<i>bovido</i>	<i>ndama ya ng'ombe</i>
ig	kusababisha kitu (-isha)	
Mf.	<i>manĝigi</i>	<i>kulisha</i>
iĝ	kuwa (-ji-)	
Mf.	<i>doktoriĝi</i>	<i>kuwa daktari</i>
il	chombo, ala	
Mf.	<i>tranĉilo</i>	<i>kisu</i>
in	Taz. uk. 35	
ind	inayostahili	
Mf.	<i>manĝinda</i>	<i>inayostahili kula</i>

ism taaluma, ufuasi

Mf. *naciismo* *Unazi*

ist Taz. uk. 57

obl Taz. uk. 39

on Taz. uk. 39

op kikundi cha idadi fulani

Mf. *duopo* *jozi*

uj chombo, mti, nchi

Mf. *Italujo* *Italia* **pomujo** *mtofaa*

ul mtu

Mf. *scienculo* *mwanasayansi*

um kinatumika kwa maana nyingine isiyojulikana

Mf. *brakumi* *kukumbatia*

Kamusi

(kwa mazoezi tu)

*** A ***

aĉet-i kununua

akr-a kali

alta -refu (urefu wa kwenda juu tu)

am-o mapenzi

am-i kupenda

amik-o rafiki

ankaũ pia

apud karibu na

arb-o mti

arb-ar-o mwitu

arimetik-o mahesabu

atent-i kuangalia

aũd-i kusikia

aũskult-i kusikiliza

av-o babu

av-in-o nyanya

*** B ***

bak-i kuoka

baldaũ hivi karibuni

ban-i kuoga

banan-o ndizi

bat-i kupiga

bazar-o soko

bel-a -zuri

benk-o deski, dawati

best-o mnyama

bild-o picha

bird-o ndege

blank-a -eupe

blu-a buluu, samawati

bon-a -ema

bon-e vema, vizuri

bot-o buti

bov-o ng'ombe dume

bov-in-o ng'ombe jike

branĉ-o tawi

bret-o rafu

brun-a hudhurungi, rangi ya maji ya kunde

*** Ĉ***

ĉambr-o chumba

ĉapel-o kofia

ĉeval-o farasi dume
ĉeval-in-o farasi jike

*** D ***

danc-i kucheza dansi
dank-i kushukuru
dank-o ahsante
dent-o jino
dev-o sharti (**taz. kifungu cha 98**)
dezir-i kutaka, kupenda
dik-a -nene
dir-i kuambia, kusema
dolĉ-a -tamu
dom-o nyumba
don-i kupa
dorm-i kulala (usingizi)

*** E ***

ebl-e labda, pengine
edz-o mume
edz-in-o mke
efektiv-e kwa kusema kweli
en ndani ya, -ni
esper-i kutumaini

*** F ***

facil-a rahisi, -isiyo tabu kufanyika
faden-o uzi
far-i kufanya
fart-
Mi ne bonfartas Siwezi
feliĉ-a furahifu, -enye furaha
fenestr-o dirisha

ferm-i kufunga
fil-o mtoto wa kiume
fil-in-o mtoto wa kike
fin-i kumaliza
fingr-o kidole
fiŝ-o samaki
flav-a rangi ya manjano
flor-o ua (maua)
flu-i kwenda kama mto
flug-i kuruka
fork-o uma (nyuma)
fort-a -enye nguvu, imara, kali
frat-o ndugu mwanamume, kaka
frat-in-o ndugu wa kike, dada
fremd-a -geni, -a nchi nyingine
freŝ-a -bichi, -tefu, -pya
frukt-o tunda
futbal-o mchezo wa mpira wa miguu

*** G ***

gaj-a -enye furaha, -enye hali ya kuchekacheka
gazet-o gazeti
geografi-o jiografia
glas-o bilauri, gilasi
grand-a -kubwa
griz-a -enye rangi ya kijivu
gvid-i kuongoza

*** Ĝ ***

ĝarden-o bustani

*** H ***

hak-i kutema

har-o unywele

hav-i kuwa na, -na

hel-a -angavu

hel-e kwa uangavu

help-i kusaikia

help-o msaada

hieraŭ jana

hok-o chango

hom-o mtu

hund-o mbwa dume

*** I ***

infan-o mtoto mdogo

ink-o wino

inter kati ya

interes-a -na-vutia, -a ku-
vutisha

ir-i kwenda

*** J ***

jar-o mwaka

juĝ-i kutoa uamuzi kortini

jun-a -changa

*** K ***

kaf-o kahawa

kaĝ-o kitundu

kajer-o daftari

kamen-o dohani

kamp-o shamba

kant-i kuimba

kap-o kichwa

kapt-i kutega

kar-a mpendwa

kaŝ-i kuficha

kat-o paka

klar-a wazi

klas-o darasa

knab-o kijana mwanamume,
mvulana

knab-in-o kijana mwanamke,
msichana

kok-o kuku

kolor-o rangi

komb-i kuchana

komb-il-o kitana

konsil-i kutoa shauri

konsil-o shauri

kontent-a -enye kuridhika

korespond-i kuandikiana
barua

kort-o bustani

krajon-o kalamu ya risasi

kret-o chaki

kudr-i kushona

kun na, pamoja na

kur-i kukimbia, kupiga mbio

kurac-i kuponya

kuŝ-i kulala chini

kuz-o mtoto mwanamume
wa ndugu wa mzazi mmo-
jawapo; binamu

*** L ***

labor-i kufanya kazi

labor-o kazi
lac-a -chovu
lamp-o taa
land-o nchi
laŭt-a -enye sauti juu
lazur-a -enye rangi ya samawati
leccion-o kipindi cha somo
leg-i kusoma
leon-o simba
lern-i kujifunza, kusoma
lern-ant-o mwanafunzi
lern-ej-o shule
lert-a stadi, -enye ufundi mkubwa
leter-o barua
libr-o kitabu
lign-o kuni
lign-a -a mti
lingv-o lugha
lini-o mstari
lit-o kitanda
loĝ-i kukalia
lok-o mahali
long-a -refu (urefu wa kwenda mbele au wa muda)
lud-i kucheza
lum-a -enye nuru
lun-o mwezi (sayari)
lund-o jumatatu

***** M *****
man-o mkono
mangŭ-i kula
mangŭ-aĵ-o chakula

map-o ramani
mar-o bahari
mard-o jumanne
matur-a -bivu
mebl-o fenicha
merkred-o jumatano
mol-a -ororo, tefutefu
monat-o mwezi (kipindi cha mwaka)
mont-o mlima
morgaŭ kesho
mort-i kufa
mur-o ukuta
muŝ-o inzi

***** N *****
nev-o mtoto wa ndugu
nigr-a -eusi
nokt-o usiku
nom-o jina
nov-a -pya
numer-o nambari, tarakimu
nun sasa
nur tu

***** O *****
objekt-o kitu
oft-e mara nyingi
onkl-o ndugu mwanamume wa mzazi; ami; mjomba
onkl-in-o ndugu mwanamke wa mzazi; shangazi
orangŭ-o chungwa
ord-o utaratibu, mpango

*** P ***

pacienc-a -enye subira, -
vumilivu
pan-o mkate
paper-o karatasi
papili-o kipepeo
parol-i kuongea, kuzungumza,
kusema
paŝt-i kuchunga
patr-o baba
patr-in-o mama
pen-i kujitahidi
pend-i kuanga, kuangikwa,
kutundikwa
pentr-i kuchora
plafon-o dari, sakafu (ya juu)
plank-o sakafu (ya chini)
plen-a -mejaliwa, -mejawa
plor-i kulia (machozi)
plum-o kalamu (ya wino)
pord-o mlango
port-i kuleta
post baada ya
poŝt-kart-o kadi ya ku-
pelekea kwa njia ya posta
pov-i kuweza
prav-a -enye haki, sahihi,
sawa
prefer-i kupenda, kupende-
lea
pren-i kuchukua, kutwaa
pret-a tayari
pun-i kuadhibu
pup-o bandia
pupitr-o meza, deski

pur-a safi

*** R ***

rab-i kuiba
rigard-i kutazama
reg-o mfalme
riccv-i kupewa
riĉ-a tajiri, -enye mali nyingi
rid-i kucheka
rigardi kutazama
ripoz-i kupumzika
river-o mto
romp-i kuvunja
roz-o waridi
ruĝ-a -ekundu

*** S ***

saĝ-a -enye busara, -a busara
salt-i kuruka, kudakia
san-a -enye afya, -zima
sci-i kujua
seg-i kupasulia kwa msumeno
seg-il-o msumeno
seg-o kiti
send-i kupeleka, kutumia
serĉ-i kutafuta
sid-i kukaa kuketi
silent-i kunyamaza
simpl-a rahisi
simpl-e tu, peke yake, bila
anasa
sincer-e -aminifu
skatol-o sanduku
skrib-i kuandika
star-i kusimama

stel-o nyota
strat-o njia (katikati nyumba
mjini au kijijini)
sub chini ya
sufiĉ-i kutosha
sur juu ya

*** Ŝ ***

ŝaf-o kondoo
ŝip-o meli
ŝlos-i kufunga kwa ufunguo
ŝtup-o kipago
ŝtup-ar-o ngazi, daraja
ŝu-o kiatu

*** T ***

tabl-o meza
tabul-o ubao
tag-o siku
tas-o kikombe
task-o kazi, sbughuli, ma-
zoezi
te-o chai
telefon-i kupiga simu
telefon-o simu
temp-o wakati
ten-i kushika
tim-i kuogopa

tranĉ-i kukata
tond-i kunyoa
tond-il-oj makasi
tre sana
trink-i kunywa
trov-i kukuta
tuŝ-i kugusa

*** U ***

urb-o mji
uz-i kutumia

*** V ***

vagon-o behewa (la gari la
moshi)
vagon-ar-o gari la moshi
varm-a -enye joto, -a moto
vart-i kulea
vart-ist-in-o yaya
vaz-o chungu
ven-i kuja
al-ven-i kufika
vend-i kuuza
ver-a -a kweli
verd-a -enye rangi ya kijani
vid-i kuona
vir-o mwanamume
voj-o njia

Faharisi

vifunguni

al 34

alama ya mtendewa 52, 56,
57, 59

apud 32

barua 104, 105

âar 66

âi 74

âiam 86

âie 91

âiuj 83

âu 36, 37, 38, 39, 40

da 51

de 21, 71

en 21

estas 20, 9, 21

for 91

heshima 100

jam 86

jen 98

jina 6

kaj 21

kia 36, 11, 59

kial 66, 36

kiam 62, 36

kiambishi 5, 6, 8, 11, 12, 14,
24, 25, 42, 52, 56, 57, 59,
60, 89, 95

kiambishi awali 5, 12

kiambishi tamati (cha
mwisho) 5, 24, 25, 42, 52,
60, 95

kiashirio 73, 7, 23, 74

kibainishi 4, 9, 19

kie 36, 23

kielezi 88, 61, 86, 89, 91

kihusishi 76

kiima 26, 52

kikati (kiambishi cha ndani)
5, 44, 68, 69, 78, 80, 84

mkazo 2

kio 36, 7, 23

kiom 51, 36

kiongezi 31, 21, 32, 33, 34, 71,
81

kionyeshi 73, 7, 23, 74

kimilikishi 64, 65

kirejeshi 76	<i>neniam</i> 86
kitenzi (na nyakati) 24, 25, 42, 60, 72, 95	<i>nenie</i> 91
<i>kiu</i> 36, 7, 11, 23, 28, 51, 552, 59, 62	<i>oble</i> 50
kiulizi 36, 7, 11, 23, 28, 51, 52, 59, 62, 66	<i>one</i> 50
kivumishi (au sifa) 8, 11, 16, 17, 48, 103	<i>per</i> 81
kiyeyusho 5	<i>plus</i> 50
kukana 21, 29	rangi 46
kutotenda 29, 21	sed 21
<i>la</i> 4, 9	siku ya juma 63
maamkio 101, 104, 105	<i>sub</i> 33
<i>mal-</i> 12	<i>sur</i> 21
matamshi 1, 3, 10	tarehe 104, 105
<i>minus</i> 50	<i>tie</i> 23, 73, 74
misemo 72, 99, 102	<i>tio</i> 7, 73, 74
mtendaji 26, 52	<i>tiu</i> 73, 74
mtendewa 52, 56, 57, 59	udogo (<i>-et-</i>) 68
uundaji wa maneno 5, 93	ukubwa (<i>-eg-</i>) 69
<i>-n</i> 52, 56, 57, 59	ulinganifu wa maneno 57, 59
nambari 46, 50	upangaji wa vivumishi 17, 48
<i>ne</i> 29, 21	wakati ujao 60
<i>ne estas</i> 21	wakati uliopita 42
	wakati uliopo 25
	wingi 14, 16, 19
	yambwa 52, 56, 57, 59

STRUKTURO DE LA ESPERANTO-MOVADO

Por efektiviĝi la agadojn, efikiĝi la agadojn, pli bone grupiĝi.

Strukturo helpas.

Jen prezento de la **Esperanto-movado**.

- Bona kono de la Esperanto-movado nepras por aktivulo.
- La plej granda organizaĵo la Esperanto-movado estas UNIVERSALA ESPERANTO-ASOCIO, **UEA**.
- La sidejo de UEA estas en Roterdamo, Nederlando.
- La organo de UEA estas la revuo *ESPERANTO*. Organo = oficiala voĉo.
- UEA organizas ĉiun jaron Universala Kongreson, UK.
- UEA havas himnon.
- Unua UK okazis en Bulonjo ĉe Maro en Francio en 1905. Poste Ĝenevo.
- Jubilea UK en Varsovio, Pollando, estis en 1987.
- Agadoj de UEA: UKoj, Retejo, Financa servo (kvazaŭ banko), Eldonejo kaj multe pli. . .
- UEA havas 7-personan estraron.
- Nova prezidanto ekde 2019 estas Duncan Chartes el Usono.
- UEA donas strukuron kaj gvidliniojn al la movado.
- Asocioj ligita al UEA estas de du specoj: **Landaj** asocioj kaj **Fakaj** asocioj.
 - 71 Landaj Asocioj, LA
 - 62 Fakaj Asocioj, FA (en 2014)
- Listo de LA kaj FA kaj listo de delegitoj troviĝas en **JARLIBRO** DE UEA.
- Landa Asocio estas asocio pri Esperanto en iu preciza lando, Ŝtato.
- En kelkaj landoj LA devas obteni agnoskon de la Ŝtato. En aliaj landoj tiu paŝo ne necesas. El tio vi komprenas, ke vi devas esplori pri tio en via lando.
- Landa Asocio organizas kongreson. Eble.
- Provu trovi Fakajn Asocioj! *Estas 62...*
 - Se vi trovas 10, vi estas sufiĉa.
 - Se vi trovas 20, vi estas bona.
 - Se vi trovas 30, vi estas tre bona.
 - Se vi trovas 40, vi estas elstara.
 - Se vi trovas 50, vi estas altnivela movadano!
- Kio estas la laboro de UEA-delegito?

- Kiel delegito mi ricevis 3 demandojn dum plimalpli 20 jaroj kaj respondis ilin.
- La junulara organizaĵo de UEA nomiĝas **TEJO**.
- TEJO organizas siajn kongresojn ĉiujare: IJK.
Aperas *KONTAKTO*.
- en “Kontakto” aperas movada rubriko “TEJO Tutmonde”.
- Genia ideo de TEJO: pasporta servo.
- UEA estas NRO ĉe UN, Unuiĝintaj Nacioj.
- UEA estas NRO ĉe Unesko.
- Kio estas NRO? Ne-Registrita Organizo
- UEA havas komisionojn laŭ la kontinentoj.
- Afrika Komisiono.
- Komisiono pri Azia kaj Oceania Esperanto Movado, KAOEM.
- Amerika Komisiono.

Esperanto en la RETO
Kiesperanto katika MTANDAO

Organizoj
Mashirika
www.uea.org
www.sat-amikaro.org
www.ilei.info
www.tejo.org

Por lerni Esperanton
Kujifunza Kiesperanto
www.duolingvo.com
www.lernu.net
www.edukado.net

Por informiĝi pri la lingvo
Kupata habari kuhusu Kiesperanto
www.esperanto.net
<https://fr.wikipedia.org/wiki/Espéranto>
<https://en.wikipedia.org/wiki/Esperanto>

Por aŭdi la lingvon en la Reto
Kusikia Kiesperanto kwenye Mtandao
www.muzaiko.info

<http://esperantaretradio.blogspot.com/>
<https://kern.punkto.info/>
<http://pola-retradio.org/>
<http://www.radiohc.cu/eo>
<http://www.radio-vatikana-esperanto.org/index.php>
<https://djpod.com/amindaesperanto>
<https://www.podkasto.net>